Jumatatu Septemba 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581801
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 21
**ANCELOTTI: MBAPPE SASA NI MPYA ZAIDI**

UKURASA 3
**Mapya** yaibuka polisi utata wa kifo cha daktari



UKURASA 5
**Aliyemuua** mke kwa kunyimwa tendo la ndoa akwama kortini

UKURASA 7
**Walimu** kikaangoni kwa kukataa kuishi nyumba za kijijini

# TEC yawakutanisha CCM na CHADEMA

• **Maaskofu** wahoji maswali magumu kuhusu utekaji... *Ukurasa 2*



Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi (kushoto), Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu (katikati) na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, wakitambulishwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima (hayupo pichani) katika kilele cha Kongamano la 5 la Ekaristi Takatifu Kitaifa lililofanyika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Daktari: Sigara na pombe si visababishi vya saratani

UKURASA 3



## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### ZITTO ACHARUKA MCHUCHUMA NA LIGANGA KUSUASUA

KIONGOZI mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema kitendo cha serikali kusuasua kukamilisha mradi wa Mchuchuma na ....

UKURASA WA 10

### AKUTWA AMEFARIKI DUNIA KANDO YA MTO

MKAZI wa Kijiji cha Kyoruba wilayani Tarime mkoani Mara, Elia Sigirya, amekutwa amefariki dunia kando ya Mto Renyamabi, huku mwili wake ukiwa na ...

## Wagumba waivaa wizara gharama za upandikizaji mimba

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA NA HESABU CBE KUFIA Z'BAR UK.24

**MAONI,** UK.6

# TEC yawakutanisha vigogo CCM, CHADEMA

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) limewakutanisha viongozi wa CCM na CHADEMA, likionya kuwa tunu za undugu na amani nchini zimeshambuliwa kutokana na matukio ya kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa Watanzania yanayoendelea.

Viongozi hao ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi.



Balozi wa Tanzania Uholanzi, Caroline Kitana Chipeta, akipongezwa na Mstahiki Meya wa Mji wa The Hague, Jan Van Hanen, kwa Tanzania kuwa kivutio kikubwa kwenye Tamasha la Mabalozi 2024 (Embassy Festival) nchini Uholanzi lililovutia watazamaji zaidi ya 50,000 mjini The Hague mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

Akiwatambulisha viongozi hao jana kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, alisema walikwenda kushiriki Kilele cha Kongamano la Tano la Ekaristi Takatifu la Kitaifa.

Padri Kitime aliwaita na kuwasimamisha kwa pamoja viongozi hao jukwaani kuwatambulisha kisha aliwakumbusha kuwa wao ni ndugu, hivyo wakaishi kwa upendo, wakapeleke tunu ya injili na kusambaza upendo katika vyama vya siasa.

Alisema historia ya viongozi inaonesha kuwa walilelewa kwenye misingi ya kikatoliki, hivyo wakaienzi Ekaristi kwa kuendeleza upendo na undugu.

Akimtambulisha Lissu, Padri Kitime alikumbusha kuwa mwaka 2017 alipokwenda kumjulia hali Nairobi alikolazwa baada ya kupigwa risasi na watu ambao mpaka leo hawajulikani na kumweleza kuwa awasamehe watu hao; naye akamjibu kuwa "Niwasamehe wakati siwajui?"

Alisema kuwa Lissu pia alimweleza kuwa Mungu yupo na ameona ukuu wake.

Katibu Kitime alisema Balozi Dk. Nchimbi alisoma Shule ya Sekondari Uru Seminari yenye maadili ya kidini huku Mnyika alisoma Shule ya Sekondari Maua Seminari.

"Ninyi nyote ni ndugu, hivyo mkaishi kwa upendo, pelekeni tunu ya injili katika vyama vya siasa," Padri Kitime alitoa malekezo hayo ya kanisa.

**KAULI YA TEC**

Akisoma salamu za TEC, Makamu wa Rais wa baraza hilo, Askofu Eusebius Nzigilwa, alisema kuwa hivi sasa tunu za undugu na amani ya nchi zimeshambuliwa kutokana na matukio ya kuteka, kutekwa, kuumizwa na kuuawa Watanzania yaliyotokea hivi karibuni.

Alisema Tanzania kwa miaka mingi inajulikana kama kisiwa cha amani, udugu na mahali pekee Afrika ambapo raia wake wameendelea kuishi kwa umoja, amani na undugu licha ya tofauti zao za kikabila, kiimani, kiitikadi na kiuchumi.

"Tunajiuliza nini kimepotea kwenye tunu yetu hii? Taifa letu limepotea wapi? Je, uongozi na mamlaka husika pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimezidiwa nguvu na maarifa hata kushindwa kudhibiti hali hii?" alihoji.

Alisema TEC haiamini kama makundi hayo ya kihalifu yana nguvu kuliko vyombo vya ulinzi na usalama na kuviomba vitimize majukumu yao, ili kurudisha heshima ya taifa ya kuwa kisima cha undugu na amani.

Alitoa pole kwa ndugu wa waliouawa na wale waliumizwa katika matukio hayo na wanaungana na taaasisi na jumuiya za kimataifa kulaani.

"Tunaunga mkono wito wa viongozi wa watu mbalimbali wa kufanyika uchunguzi wa kina na haraka, ili wale wote waliohusika na matukio hayo yafikishwe mbele ya sheria," alisema.

Alisema pia wanakemea vitendo hivyo vya kihalifu na kuunga mkono wito wa viongozi na watu mbalimbali wa kufanyika uchunguzi wa kina na haraka, ili waliotekeleza vitendo hivyo wafikishwe mbele ya sheria na wale ambao hawakuwajibika kwa kadili ya nafasi zao wawajibishwe.

"Uhai ni zawadi kutoka kwa Mungu, mtu ameumbwa kwa sura na mfano Mungu mwenyewe, hivyo maisha na utu wa mtu ni lazima viheshimiwe na kulindwa kwa nguvu zote," alisema.

Septemba 8, mwaka huu, mara baada ya kuripotiwa kifo cha Mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA Taifa, Ali Kibao, Rais Samia Suluhu Hassan alituma salamu za pole kwa viongozi wa chama hicho, familia, ndugu, jamaa na marafiki huku akiagiza vyombo vya uchunguzi kumpelekea haraka taarifa ya kina kuhusu tukio hilo na mengine ya namna hiyo.

"Nchi yetu ni ya kidemokrasia na kila raia ana haki ya kuishi. Serikali ninayoiongoza haivumilii vitendo vya kikatili vya namna hii," alisema.

Mwili wa Kibao uliokotwa katika eneo la Ununio wilayani Kinondoni baada ya kutekwa na watu wasiojulikana ndani ya basi la Tashriff wakati akitoka Dar es Salaam kwenda Tanga. Kwa mujibu wa mashuhuda waliokuwa katika basi hilo, watu waliokuwa na bunduki na pingu.

Mbali na Kibao, kumekuwa na matukio ya watu kutekwa, kuuawa na kujeruhiwa na watu wasiojulikana yanaripotiwa mara kwa mara, hata kutishia amani na kuwaibua wanaharakati na viongozi mbalimbali kuyakemea.

Rais wa TEC, Askofu Wolfgang Pisa, alisema amefurahishwa kuwaona viongozi hao wa vyama vya siasa wamekaa pamoja, jambo linaloonesha kuwa kuna nguvu ya kuwaweka watu pamoja katika Ekaristi.

**KAULI YA BITEKO**

Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, alisema maadhimisho ya Ekaristi hiyo yawakumbushe Wakristo na Watanzania wote kuishi kama ndugu kwa kuhurumiana na kutoruhusu tofauti za mitazamo ziwatenganishe na kuwagombanisha.

Alisema nchi itajengwa kwa pamoja kupitia uongozi na kusisitiza siasa za kustahimiliana na kuvumiliana, zenye lengo la kubadilisha hali za Watanzania kwa kuwaondoa katika umaskini na kuwatengenezea hali bora.

Dk. Biteko pia alitoa wito kwa Watanzania kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kujiandikisha katika Daftari la Wakazi kuanzia Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu. Uchaguzi huo utafanyika Novemba 27, mwaka huu.

"Yule atakayegombea na atakayekwenda kumpigia kura mwenzake, tufanye hivyo kwa kusaidiana huku tukijua kuwa hatuna pa kwenda," alisema.

Viongozi wengine walioshiriki maadhimisho hayo ni pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila na Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda.

# Mwigulu aeleza chanzo miradi kusuasua

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

WAZIRI wa Fedha na Mipango amesema kusuasua kwa baadhi ya miradi nchini kumetokana na kushuka kwa upelekaji fedha katika miradi hiyo, hatua iliyosababishwa na majanga mbalimbali yaliyotokea hivi karibuni na kuharibu utaratibu wa bajeti.

Dk. Mwigulu Nchemba aliyasema hayo wakati akijibu ombi la Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Johari Samizi, kuhusu kusuasua kwa miradi ya maji pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Jamii alipoanza ziara yake ya siku saba mkoani Mwanza.

Waziri huyo alisema majanga mbalimbali yaliyotokea nchini, yakiwamo mafuriko yaliyosababishwa na mvua ya El-nino, maporomoko ya Hanang', Mbeya, Lindi na Mtwara, yaliharibu mtiririko wa fedha zilizopangwa katika bajeti ya 2023/24.

"Kumekuwa na mtiririko hafifu wa utolewaji fedha katika baadhi ya miradi, hii ni kutokana na majanga hayo yaliyoathiri bajeti yote ya mwaka jana na kusababisha serikali ianze kuhudumia maeneo hayo ikiwa ni mamoja na kurejesha miundombinu na makazi ya watu ambako haikuwa imepangwa," alisema Dk. Mwigulu.

Alisema kuwa tayari wizara hiyo imewasiliana na Wizara ya Maji ambayo muda si mrefu itaanza kusambaza fedha hizo ili miradi iliyokwama ikamilishwe.

Waziri huyo alisema ipo pia miradi ya kimkakati, ikiwamo Reli ya Kisasa (SGR), Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere ambalo limekamilika kwa zaidi ya asilimia 98 pamoja na ujenzi wa daraja refu la J.P.Magufuli (Kigongo-Busisi), yote imeelekezewa zaidi fedha ili ikamilike kwa wakati na kuanza kutumika mara moja.

"Katika hili, ninadhani tumeona sasa kuwa tulikuwa na mgawo wa umeme, lakini kwa sasa umeanza kuwa historia, safari za treni ya umeme tayari zimeanza, zikiashiri uwekezaji mkubwa ulielekezwa huko na pia daraja muda si mrefu linakamilika," alisema.

Waziri Mwigulu alisema miradi hiyo imesababisha pia kupunguza upelekaji fedha katika baadhi ya miradi.

Waziri huyo ametembelea na kukagua ujenzi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kanda ya Ziwa, chuo ambacho ujenzi wake ulianza Januari 22, 2022 ukigharimu zaidi ya Sh. bilioni 7.8.

Akizungumzia ujenzi wa kampasi hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu (TIA), Prof. William Pallangyo, alisema umefikia asilimia 99 na kukamilika kwake kutasaidia kuwahudumia kwa wingi wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa.

# Mapya yaibuliwa polisi utata kifo cha daktari

**Na Vitus Audax**

JESHI la Polisi limesema aliyekuwa Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Ulyankulu, wilayani Kaliua, mkoani Tabora, Dk. Dismas Chami (32), aliwahi kujaribu kujiua mara mbili kabla ya kifo chake chenye utata kilichoripotiwa mwishoni mwa wiki.

Vilevile, jeshi hilo limesema mwili wa daktari huyo anayedaiwa kupotea kisha kukutwa kichakani amefariki dunia katika eneo la Kombo Masai, Kata ya Malolo, mkoani humo, mwili ulikutwa umedungwa dripu yenye dawa ambayo bado haijafahamika.

Katika taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa juzi na Msemaji wa Polisi Makao Makuu Dodoma, DCP David Misime, ilieleza kuwa wanaendelea na uchunguzi kwa kushirikiana na wataalamu wengine ili kubaini chanzo cha kifo cha tabibu huyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa mujibu wa uchunguzi wa awali juu ya kifo cha daktari huyo, alishajaribu kujiua mara mbili.

Jeshi hilo limesema kuwa Dk. Chami aliaga kwa mkuu wake wa kazi pamoja na mke wake Septemba 2, mwaka huu kuwa anakwenda mjini Tabora kushughulikia akaunti yake ya benki ambayo ilikuwa na changamoto.

Baada ya kuaga, jeshi hilo limeeleza kuwa Dk. Chami aliahidi kurejea siku iliyokuwa inafuata na ilipofika Septemba 4 mwaka huu, simu yake haikupatikana.

"Septemba 10, daktari mkuu wa kituo hicho cha afya aliambatana na mke wa marehemu hadi kituo cha polisi kutoa taarifa ya kutokuonekana kwake," ilieleza taarifa hiyo.

Jeshi hilo lilisema kuwa siku hiyo hiyo walitoa taarifa kituo cha polisi, Dk. Dismas alimtumia mke wake ujumbe kupitia WhatsApp ulisema:

"Nisamehe sana, baada ya dakika chache sitakuwa nanyi duniani, simamia kila kitu nilichoanzisha. Pesa zote zipo akaunti ya CRDB, simamia na watoto waseme, kwa heri."

Kamanda Misime alisema daktari huyo hakupatikana tena katika mawasiliano yake mpaka Septemba 13 majira ya saa tatu usiku, mwili ulipokutwa kichakani.



Wafanyakazi wa kampuni inayojenga barabara ya Ruangwa – Nanganga (Km 53.2) kwa kiwango cha lami na daraja la Lukuledi lenye urefu wa mita 60 mkoani Lindi wakisuka nondo kwa ajili ya daraja hilo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alipokagua ujenzi wa barabara hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: UJENZI**

# Daktari: Sigara, pombe si visababishi vya saratani

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Prudence Kiwia kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) amesema pombe na sigara si vyanzo vya saratani; wengi wanaougua hawakuwahi kutumia vilevi hivyo.

Amesema saratani zinazoongoza kila mwaka ni za shingo ya kizazi na matiti kwa wanawake na tezi dume kwa wanaume, hivyo jamii inatakiwa iwe na tabia ya kufanya uchunguzi kila wakati.

Dk. Kiwia alisema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kupokea msaada wa vifaa mbalimbali na mashine kutoka Taasisi ya Jema Foundation iliyotembelea taasisi hiyo kwa ajili ya kuwafariji wagonjwa.

"Tumefurahi sana tumepokea misaada mingi kwa wagonjwa wetu, lakini kubwa ningependa kusisitiza wananchi kwa ujumla kwa sababu saratani ni hatari sana na njia bora ya kujikinga na saratani ni kufanya uchunguzi.

"Visababishi vingi vya saratani havionekani, wengi wanaongelea pombe na sigara, lakini si anayevuta sigara na kunywa pombe ndiye anaishia kupata saratani, hapana! Tuna wagonjwa wengi wanapata saratani, hawajawahi kutumia (sigara au pombe) alisema Dk. Kiwia.

Aliwataka wananchi kufanya uchunguzi mapema wanapoona mabadiliko yoyote kama vile uvimbe au kupata uchafu sehemu za siri.

"Kwa mwaka tunapata wagonjwa wengi sana, hasa shingo ya kizazi, maziwa kwa wanawake na kwa wanaume tezi dume, hao ni wengi sana, siwezi kukupa hata mfano kulinganisha na saratani zingine kama mfumo wa chakula, kichwa... ni wachache sana," alisema.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Jema Foundation, Jema Baruan, alisema alikuwa mgonjwa wa saratani na alipona miaka minane iliyopita, na kwamba aligundulika kuwa na maradhi ya saratani ya mitoki inayoadhimishwa kila mwaka Septemba 15. Alisema wameamua kuwatembelea wagonjwa wenye saratani ili kuwapa faraja na matumaini na pia wamewapelekea baadhi ya mahitaji yakiwamo magongo, viti vya wagonjwa, mashine ya sukari, mashine ya kupima mapigo ya moyo (BP) na vitu vingine.

"Nimepitia hivi, ninamshukuru Mungu nimeweza kuikabili saratani ya mitoki na nimepona, lakini yupo mwingine ambaye anapambana na ni Mtanzania kama mimi, nikaona si haba na yeye tuje tumguse kwa sababu matendo ya huruma ndiyo matendo yanayompendekeza Mungu.

"Asilimia kubwa hawaponi lakini kuna asilimia ndogo iliyobakia wanapona, mimi nilifanya tiba ya chemotherapy ambayo ilikuwa na mizunguko 16, sikuacha tiba katikati, nilikuwa nakula ipasavyo unakuta mtu anafanya tiba, lakini hali chakula ipasavyo, tiba inamzidia," alisema Baruan.

Alisema mgonjwa anatakiwa ale vizuri na kufanya mazoezi pamoja na kusikiliza ushauri wa daktari, akionya kuchanganya huduma za hospitalini tiba za kienyeji.

"Mimi nilijikita kwenye tiba niliyoambiwa, nikafanya mazoezi, nikala vizuri nilikuwa ninajilazimisha kula, changamoto ilikuwa kwenye kula, mgonjwa unatakiwa ujilazimishe kula, bahati nzuri nimepona," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Big Bon, Ahmed Salum alisema wagonjwa wa saratani wanateseka, hivyo wameona kuwachangia chochote kwa kuwaonesha upendo.

# Wananchi wajawa hofu ya kijiji chao kufutwa

**Na Kulwa Mzee**

WANANCHI wa Kijiji cha Ngombo, Kata ya Biro, wilayani Malinyi, mkoani Morogoro wameomba serikali kuwasaidia wasihamishwe katika kijiji chao walichoishi babu zao kwa zaidi ya karne tatu baada ya kuambiwa ni wavamizi wa eneo hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar Es Salaam jana, baadhi ya wawakilishi wa kijiji hicho walidai wako katika eneo hilo kwa muda mrefu - kizazi na kizazi na wanashangaa kuambiwa wahame na mamlaka za hifadhi kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji.

"Kumekuwa na tetesi kuwa mamlaka zinazosimamia maeneo ya hifadhi zinawataka wanakijiji kuondoka kijijini haraka iwezekanavyo na hii inatutia wasiwasi kwa sababu kama kweli hilo lipo, basi lingekuja kwa kufuata taratibu za kisheria," alisema mmoja wa wanakijiji hao, Ananias Patitu.

Alieleza hofu yao ilivyo kubwa na kuomba serikali iwasaidie wasiondolewe katika maeneo yao kwa kuwa hawajui wapi wataishi ikiwa wataondolewa.

"Tunaiomba serikali ituonee huruma na kutuacha tuishi hapa kwa kuwa tupo tangu miaka mingi na tumerithi kijiji hiki kutoka kwa babu zetu ambao nao walirithi kwa babu zao," alisema Mzee Patitu.

Alisema kumekuwa na madai ya kuharibu chanzo cha maji cha Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere kupitia shughuli mbalimbali kikiwamo kilimo na ufugaji, huku wakieleza kuwa wananchi wanaelewa umuhimu wa vyanzo hivyo na hakuna uharibifu wowote uliofanyika.

Mwakilishi mwingine wa kijiji hicho, David Mkumba alisema kuwa kwa muda wote ambao wameishi kijijini huko wamewekeza vya kutosha na kijiji chao kimekuwa miongoni mwa vijiji vinavyochangia mapato kwa serikali.

"Hiki kijiji chetu kimesajiliwa na tumefanikiwa kujenga huduma zote muhimu za kijamii kama vile shule na kituo cha huduma ya afya," alisema Mzee Mkumba.

# DC akemea mmomonyoko wa maadili

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Kheri James amewaomba viongozi wa dini kuongeza nguvu kukemea na kupiga vita vitendo vyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani pamoja na mmomonyoko wa maadili vinavyochochea uhalifu na watu kukosa utu.

Kiongozi huyo alikutana na viongozi wa dini katika kikao maalum cha kujadili masuala mbalimbali, yakiwamo maadili na malezi, akitumia kikao hicho kuwaomba viongozi wa dini kusimama kidete katika nafasi zao kufundisha waumini wao namna wanavyoweza kuishi kwa kuukataa ubaya.

Alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na viongozi wa dini katika kurekebisha jamii kupitia mafundisho yao.

James alihimiza pia ushiriki wa wananchi katika miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao ili miradi hiyo iwe endelevu.

"Nimeona nikutane na ninyi viongozi wa dini ili tukumbushane mambo kadhaa yanayohusu jamii yetu ya Iringa. Miongoni mwa mambo hayo ni kuwashukuru kwa kazi mnayoendelea kufanya ya kuwahudumia wananchi na waumini wenu kiroho.

"Lakini kubwa ni kuwaomba viongozi wa dini mwendelee kuwahubiria waumini wenu kuhusu ulinzi wa amani na mustakabali wa taifa letu.

"Kama mnavyojua, nchi yetu ni mfano wa kuigwa kwa kudumisha amani na hii inatokana na umoja na mshikamano tulionao, hivyo ni wajibu wenu kuendelea kuwafundisha watu sababu za uwapo wa amani kama hii," alisema James.

Baadhi ya viongozi wa dini walioshiriki katika kikao, akiwamo Mchungaji Nickson Kawage kutoka Huduma ya Wapo Mision Tawi la Iringa, walisema kuwa miongoni mwa mambo yanayochangia amani kupotea ni watu kukosa hofu ya Mungu.

Pia alisema mmomonyoko wa maadili unaotokana na utandawazi, unachangia hatari hiyo, hivyo viongozi wa dini wataendelea kukemea kwa nguvu vitendo hivyo.

"Ni kweli sisi kama viongozi wa dini tunao mchango mkubwa wa kuhakikisha dunia inakuwa mahali salama pa kuishi, watu waishi kwa misingi ya Mungu na wapendane na kuchukuliana, watu waishi kwa kufuata misingi ya Kitanzania, hivyo tutaendelea kufundisha kama ilivyo desturi yetu wamgeukie Mungu, waishi kwa upendo," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Iringa, Tiniel Mbaga, alisema mchango wa viongozi wa dini ni mkubwa kuhakikisha jamii inakataa vitendo vyote vya kikatili na uvunjifu wa amani.

"Kikao hiki ni muhimu kwa sababu jitihada zinazofanywa na serikali zinapaswa kuwa za pamoja, hivyo kukutana pamoja na kujadili namna tunavyoweza kushirikiana ni jambo zuri lililoonesha ushindi iwapo kila mmoja wetu atatekeleza wajibu wake ipasavyo," alisema Mbaga.




Mkazi wa Mkoa wa Tanga, Amina Mfundo, akionesha bango lenye ujumbe unaohamasisha uchaguzi wa serikali za vijiji, vitongoji na mitaa, wilayani Handeni juzi, utakaofanyika Novemba 27 nchi nzima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Wawekezaji shule binafsi wawekeze kwa walimu wenye viwango bora'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

UONGOZI wa Mkoa wa Pwani umewataka wawekezaji binafsi wa shule kwenda sambamba na uwekezaji wa walimu bora watakaowezesha kuwa na wanafunzi wa kuwashindanisha kimataifa.

Katibu Tawala Mkoa huo, Rashid Mchata aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wananchi walioshiriki mahafali ya 19 ya Shule za Awali na Msingi za Kibaha Independent (KIPS) yaliyofanyika Msangani, wilayani Kibaha.

Katika hotuba yake, Mchata alisema serikali inasisitiza sekta binafsi zilizowekeza katika elimu kuhakikisha wanapata walimu bora watakaozalisha wanafunzi watakaomudu kushindanishwa ndani na nje ya nchi.

Katibu Tawala huyo alisema serikali inaendelea kuunga mkono sekta binafsi huku akiwakumbusha wazazi na walezi wa watoto wanaosoma shule binafsi kuzingatia mikataba wanayokubaliana na wamiliki wa shule kwa kuepuka kuwa chanzo cha kukwamisha mipango ya shule.

Alisema wakazi wa Mkoa wa Pwani wanatakiwa kuzingatia kuwaelimisha watoto wao kwa bidii ili wanufaike na fursa za ajira kwenye viwanda vinavyojengwa mkoani mwake.

Alisema kuwa katika shule za serikali, maboresho yanaendelea kufanyika huku ufaulu ukiendelea kukua sambamba na kuwa na mipango ya baadaye ya walimu bora watakaofundisha wanafunzi wa kukidhi viwango vya kimataifa.

Katibu Tawala huyo alisema wananchi wanatakiwa kuwa na ushirikiano na halmashauri zao na kuchangia katika ulipaji kodi zitakazojenga miradi ya barabara na kuondoa usumbufu hususani kipindi cha mvua.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Adinani Livamba, alisema wanaoamua kuanzisha shule binafsi wahakikishe wanakuwa na uwekezaji wenye tija kwa kuwa na walimu bora na si wale waliokosa ajira na kuamua kuwa walimu kama sehemu mbadala.

Mkurugenzi wa Shule za KIPS, Yusuph Mfinanga, aliwaomba wazazi kulipa ada kwa wakati ili mipango yao ikamilike kwa wakati huku akiahidi kusomesha bila malipo wanafunzi 15 kwenye Shule za Vuchama na Mangio kutoka shule za KIPS watakaoibuka na ufaulu wa alama A.

Mmoja wa wazazi wa wahitimu hao, Emmanuel Kulaya, alisema kila mzazi anatakiwa kuchukua nafasi yake kulinda maadili ya watoto wao wasijiingize kwenye makundi yasiyofaa, huku akiwakumbusha kujenga tabia ya kushirikiana na walimu na kufuatilia maendeleo ya watoto wao.

## Wajasiriamali wapewa mbinu kupenya EAC

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye ubora ili waweze kushindana katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na hata Ulaya na Amerika.

Imeelezwa kuwa mashirika ya viwango ya nchi za EAC yameingia makubaliano, ambapo bidhaa ikishathibitishwa ubora na shirika la viwango la nchi husika, haitakiwi kupimwa tena inapopelekwa kwenye soko la nchi nyingine.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uthibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Sileja Lushibika, wakati akitoa elimu kwa wajasiriamali 46 pamoja na wananchi kwenye maonesho ya saba ya mifuko ya programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Maonesho hayo yalifanyika mkoani Singida katika Viwanja vya Bombadier kuanzia Septemba 8 hadi 14, mwaka huu.

"Kupitia maonesho haya tunawaeleza wajasiriamali kwamba kwa sasa tupo kwenye soko la EAC ambapo mashirika ya viwango ya nchi hizo yameelewana kwamba bidhaa zinazozalishwa nchi mojawapo zinaweza kwenda nchi yoyote bila kulazimika kupimwa tena.

"Tunahakikisha wajasiriamali wadogo wanaendelea, serikali inagharamia kuthibitisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali na kuendelea kuhudumiwa kwa miaka mitatu tukiwa na imani kwamba baada ya hapo watakuwa wamekua na kufikia mahali fulani," alisema Lushibika.

Alisema TBS itaendelea kuhakikisha wajasiriamali wanapata elimu ya kupata alama ya ubora kwa kuwa inawezekana wengine hawajui kuwa kupata alama kumerahisishwa.

"Lakini wote walioshiriki maonesho haya wanapokuja hapa wanapata elimu ya namna ya kupata alama ya ubora, tunawapa kanuni bora za usindikaji kwani kuna vitu vya msingi ili bidhaa iweze kuwa bora kuna kanuni wanatakiwa wazifuate," alisema Lushibika.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kuchangamkia fursa ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure kwa kuwa hivi sasa utaratibu wa kutuma maombi umerahisishwa, ambapo maombi yanatumwa kwa njia ya mtandao.

Alisema wajasiriamali wanatakiwa kuwa na barua ya utambulisho kutoka Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) wanapowasilisha maombi ya kuthibitisha bidhaa zao.

Maonesho hayo yalifunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi.

# Wagumba wataka kipaumbele kupandikiza mimba Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wagumba Tanzania kimewasilisha hoja katika Wizara ya Afya na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kiwe kundi la kwanza kupata huduma ya upandikizaji mimba (IVF) iliyozinduliwa Alhamisi iliyopita katika hospitali hiyo.

Kundi hilo pia linaomba serikali na wadau wengine wa afya kuwasaidia kuchangia gharama ya upatikanaji huduma hiyo ambayo ni Dola za Marekani 5,000 (sawa Sh. 13,611,700) kutokana na wengi wao kuwa na kipato kidogo.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki ikiwa ni siku chache baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kuzindua jengo la IVF hospitalini huko, Mwenyekiti wa chama hicho, Shamila Makwenjula, alisema kundi hilo linapitia changamoto kadhaa ikiwamo katika afya ya akili.

"Hospitalini tiba za uzazi ziko juu. Katika chama chetu kuna takribani wanachama 60, wamo pia wanaume. Serikali inapochangia gharama nyingine, basi isaidie na kundi hili.

"Tuliuliza huduma za upandikizaji hospitali binafsi ilikuwa karibu Sh. milioni 20. Muhimbili bei imeshuka kidogo, lakini kuna mtu hata Sh. milioni moja hajawahi kuishika.

"Ummy Mwalimu alitupokea, sasa Jenista Mhagama (Waziri wa Afya), apokee kilio chetu serikali itusaidie kwamba sisi tutachangia kiasi kidogo. Kuna wengine wana ugumba ila hawajapata matibabu sahihi, wakitibiwa watapata watoto.

"Kuna huduma za kliniki za umma za magonjwa mengine, kama yasiyoambukiza, lakini ugumba umewekwa kando," alisema. Mwenyekiti huyo alisema jamii ina dhana potofu ambazo wanakumbana nazo kama vile kuonekana ni watu walio na mkosi, wasio na tija, huku baadhi wakichukua uamuzi mgumu kwa kutaka kujitoa uhai au kuiba watoto.

Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Idara ya Afya ya Akili Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), Dk. Raymond Mgeni, anasema kundi hilo hukumbwa na magonjwa ya akili kutokana na wengi wao kunyanyapaliwa.

"Unyanyapaa wanaopata unawaletea athari za wengi kujikuta wakiwa katika msongo wa mawazo ambao unachochea sana wengine kujiua, kunywa pombe na sonona pia," anasema Dk. Mgeni.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema tayari huduma hiyo imeanza na kliniki kwa kinamama 10 ili kupandikizwa, na kwamba kila siku kati ya wagonjwa 10 wanaoonwa katika kliniki ya kinamama, watatu hadi wanne wana tatizo la uzazi sawa na asilimia 30.



Mwenyekiti wa Bodi ya Young Scientists Tanzania (YST), Profesa Yunus Mgaya, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu maandalizi ya maonesho ya kitaifa ya YST yatakayofanyika Septemba 19, jijini Dar es Salaam. kushoto ni Mwanzilishi Mwenza wa Young Scientists Tanzania (YST), Dk. Gozibert Kamugisha na kulia ni Ofisa Mtendaji wa Taasisi ya Karimjee Foundation, Caren Rowland. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aliyemuua mkewe kwa kunyimwa tendo la ndoa ashindwa rufani

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imetupilia mbali rufani iliwasilishwa na Erick Buberwa aliyefungwa miaka minane kwa kumuua bila kukusudia mkewe kwa kumnyima tendo la ndoa kwa sababu haina mashiko.

Hukumu hiyo ya mahakama ilitolewa juzi Mahakama ya Rufani Dar es Salaam mbele ya jopo la majaji watatu; Jaji Ferdinand Wambali, Jaji Lilian Mashaka na Jaji Benhaji Masoud baada ya kupitia hoja za pande zote mbili.

Mrufani Buberwa aliwasilisha rufani dhidi ya Jamhuri, akipinga adhabu ya kifungo cha miaka minane alichohukumiwa na Mahakama Kuu kwa kumuua bila kukusaidia mkewe Mercy Mukandala Juni, 2020.

Ilidaiwa mahakamani kuwa Juni 16, 2020, huko Kimara, majira ya usiku, mrufani na mkewe, wakiwa chumbani wamelala, mrufani aliomba kupewa haki yake ya ndoa lakini mkewe alikataa kumpa.

Inadaiwa katika kutofautiana huko, alimwambia mkewe ana mwanamume mwingine anayempenda kuliko yeye kisha akainuka kuelekea jikoni na kurudi na spana ya kufungulia bomba akiwa na lengo la kumpiga nayo mrufani, badala yake mrufani alimpigia nayo mkewe kichwani.

Mkewe aliangukia meza huku akiwa na jeraha, alivuja damu, mrufani aliwafahamisha majirani; walimchukua kumpeleka hospitali lakini alifariki dunia akiwa njiani.

Inadaiwa mrufani aliripoti polisi na mwili wa marehemu ulipelekwa Hospitali ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) kwa ajili ya uchunguzi ambako kifo chake kilibainika kusababishwa na majeraha kichwani yaliyosababisha kuvuja damu na kupoteza maisha.

Mrufani alifikishwa mahakamani kwa mashtaka ya mauaji ya bila kukusudia na baada ya usikilizwaji, alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka minane gerezani kwa kuua bila kukusudia.

Baada ya adhabu hiyo, mrufani aliwasilisha rufani mahakamani akipinga adhabu akiwa na sababu mbili; kwanza ni kwamba mahakama haikuzingatia kwamba ni mkosaji wa mara ya kwanza na haikuzingatia maombolezo yake ya kupunguziwa adhabu.

Sababu ya pili anadai mahakama haikuzingatia kwamba kifo kilitokana na kunyimwa haki yake ya ndoa na maneno yaliyotamkwa na marehemu kuwa ana mwanamume mwingine anayempenda zaidi yake.

Mrufani katika usikilizwaji aliwakilishwa na Wakili Musa Mhagama huku wajibu rufani wakiwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Job Mrema, akisaidiana na Wakili wa Serikali John Mwakifuna.

Wakili Mhagama aliomba kuondoa sababu ya pili na kubakia na sababu ya kwanza kwamba mazingira ya utendaji kosa hayakuzingatiwa na mahakama haikuzingatia kuwa mrufani amebaki na jukumu la kulea mtoto wao mdogo.

Alijibu hoja za rufani, Wakili Mrema alidai mahakama ilitenda haki kisheria, ilizingatia mazingira yote ya utendaji kosa na kwamba aliomba Mahakama ya Rufani imwongezee adhabu mrufani kutoka miaka minane jela hadi miaka 20 jela.

Baada ya kusikiliza hoja za pande mbili, jopo lilisema kwamba kabla ya kuhitimisha, wanaona inafaa kutoa maoni yao kwa mwaliko uliotolewa na Wakili Mrema kwamba mahakama iitishe maombi yake kwa mamlaka iliyonayo kisheria kuongeza kifungo cha miaka 10 impe mrufani kifungo cha miaka ishirini jela.

"Sisi kwa heshima tunakataa mwaliko wa Wakili Mrema, kwa maoni yetu Jamhuri ambaye ni mlalamikiwa ilipaswa kuwasilisha rufani mtambuka kama alikuwa hakuridhishwa na adhabu.

"Hakuna rufani nyingine mbele yetu. Hivyo, hatuoni sababu ya kuingilia kati hukumu ya Mahakama Kuu. Kwa kusema hayo, mwombaji anapaswa kutumikia kifungo cha miaka minane kilichotolewa na Mahakama Kuu," lilisema jopo.

Mahakama ya Rufani iliona rufani haina mashiko, hivyo ikatupiliwa mbali.

## INEC yawapa angalizo watendaji uboreshaji Daftari la Wapigakura

**Na Mwandishi Wetu**

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imewataka watendaji wa uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura kutekeleza majukumu yao kwa umakini katika kila eneo, ukiwamo utunzaji vifaa vya uandikishaji.

Wito huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji wa Mahakama ya Rufani (mstaafu), Mbarouk Salim Mbarouk, wakati akifungua mafunzo ya watendaji wa uboreshaji daftari hilo ngazi ya mkoa na halmashauri za mkoa wa Dodoma.

"Vifaa hivi (vya uboreshaji daftari) vimenunuliwa kwa gharama kubwa sana na vinatarajiwa kutumika katika maeneo mengine ya uandikishaji nchini. Kutokuwa makini katika utunzaji vifaa hivi kutapelekea athari kubwa katika ukamilishaji wa zoezi hili muhimu," alionya.

Aliwataka watendaji hao kuzingatia maelekezo yote yatakayotolewa na INEC ili wayafanyie kazi wakati zoezi litakapokuwa limeanza.

Akifungua mafunzo kama hayo mkoani Singida, Mjumbe wa Tume hiyo, Dk. Zakia Mohamed Abubakar, alisema matokeo bora ya zoezi la uboreshaji wa daftari yatatokana yanategemea kuwapo ushirikiano mkubwa kati ya watendaji wote wa uboreshaji, serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi.

"Ninawasihi muwe na ushirikiano mzuri na wa karibu na tume wakati wote mtakapokuwa mnatekeleza majukumu yenu na ikiwa mnahitaji ufafanuzi au maelekezo yoyote, msisite kuwasiliana na tume," alisema mjumbe huyo.

INEC pia imewataka mawakala wa vyama vya siasa kutowaingilia watendaji wakati wote wa utekelezaji maboresho ya daftari.


Dk. Zakia alisema wakati wa uboreshaji daftari, mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwapo katika vituo vya kuandikisha wapigakura ili kuleta uwazi katika zoezi hilo.

"Mawakala hao watasaidia kutambua waombaji wa eneo husika na hivyo kupunguza kutokea kwa vurugu zisizokuwa za lazima lakini hawaruhusiwi kuwaingilia watendaji wakati wakitekeleza majukumu yao vituoni," alisema.

Alisema tume ilishatoa kibali kutoa elimu ya mpigakura wakati wa uboreshaji daftari kwa asasi za kiraia 157 na asasi nyingine 33 zitahusika kwa ajili ya uangalizi wa zoezi hilo.

Mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni maandalizi ya mzunguko wa tano wa uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura ambao utajumuisha mkoa wa Dodoma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Kongwa, Mkoa wa Manyara katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Wilaya ya Kiteto na Simanjiro na mkoa wa Singida.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




## TFF, TPLB msiwalazie damu waamuzi hawa Ligi Kuu Bara

**KAMA** hali itaenda kama inavyoonekana juzi basi Tanzania tuna safari ndefu kuelekea kwenye mafanikio halisi ya soka pamoja na serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ili soka letu liwe juu.

Licha ya serikali kuweka mazingira mazuri, klabu kufanya uwekezaji kwa kusajili wachezaji bora na miundombinu kuendelea kuboreshwa, kunatakiwa kuwapo kwa usimamizi mzuri kutoka kwa viongozi wa soka, pamoja na waamuzi.

Waamuzi pamoja na kwamba huwa wanasahaulika, lakini na wao wanachangia sana kupandisha au kushuka kiwango cha soka cha nchi husika kwa jinsi watakavyokuwa wanatoa maamuzi yao kwa sababu ni hao hao wanaweza kuipa ubingwa timu isiyostahili halafu ikaenda kuchekesha kwenye michuano ya kimataifa.

Ligi ya Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya nne kwa baadhi ya timu, zingine zikiwa hazijamaliza raundi ya tatu, lakini tayari tumeshaanza kuona vituko vya waamuzi kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia misimu iliyopita.

Mwamuzi Tatu Malongo juzi katika Uwanja wa Azam Complex, aliwashangaza wengi alipokataa bao la Pamba Jiji FC lililoonekana ni halali kabisa.

Benny Nakibinge aliukwamisha mpira wavuni dakika za majeruhi, ila mwamuzi alionekana kubabaika katika maamuzi yake, licha ya mwamuzi msaidizi kuwa ameshaondoka kwenda kati ikiwa ni ishara ya kulikubali bao hilo, lakini cha ajabu baadaye ilionekana mpira ukiwekwa faulo nje kidogo ya eneo la hatari.

Alikuwa ni Salehe Masoud aliyempasia, George Mpole ambaye alikatwa nje kidogo ya eneo la hatari, lakini mpira uliendelea kuzagaa zagaa ukiwa kwenye himaya ya Pamba, Nakibinge akaukwamisha wavuni.

Tunaamini lilistahili kuwa bao kwa sababu aliyefanyiwa faulo alikuwa mchezaji wa Pamba na bado mpira walikuwa wanaumiliki wao hivyo mwamuzi akatoa faida kwao ya kuendelea na mpira, lakini bao lilipofungwa akalikataa na kuamuru ipigwe faulo baada ya majadiliano marefu na mshika kibendera.

Tunadhani hapa kuna mawili. Moja Malongo inaonekana alikuwa mbali na tukio, hivyo hakujua nini kimetokea kwa Mpole kuanguka chini. Huku ikionekana pengine awali alidhani labda amejiangusha, akaonyesha mpira upigwe kuelekea Pamba, baadaye akatoa faulo nje ya eneo baada ya kujua ameangushwa.

Lakini kwa nini hakumsikiliza mwamuzi mwenzake wa pembeni aliyekuwa amelikubali bao kwa kuwa yeye alikuwa karibu zaidi na tukio? La pili inawezekana Mwalongo alikuwa anataka mechi iishe sare kwani zilikuwa ni dakika za majeruhi kwani ilionekana si rahisi kwa Azam kurudisha bao kwa muda huo.

Tumekuwa tukishuhudia maamuzi mabovu kama hayo, hasa mara nyingi timu kubwa zinapofunga mabao dakika hizo hukubaliwa na waamuzi na haitakiwi kuwa hata na shaka yoyote, kwani litasimama kuwa bao tu.


Tunadhani umefika wakati Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), kuchukua hatua za makusudi juu ya uchezeshaji huu usiokuwa wa kiungwana.

Timu kama Pamba ndiyo kwanza imepanda baada ya miaka 23 ya kusota, leo bao lao linakataliwa kikatili, na kukosa pointi tatu. Je, mwisho wa siku ikishuka daraja kwa tofauti ya pointi moja mwishoni mwa msimu si itakuwa imeshushwa na maamuzi mabovu ya waamuzi kama hawa?

Uchezeshaji huu ndiyo unazifanya baadhi ya timu kubebwa isivyo hali na kwenda kushiriki michuano ya kimataifa wakati hazina uwezo, matokeo yake zinatolewa na timu dhaifu zenye kariba ya Pamba Jiji hiyo hiyo na mashabiki wanashangaa. Kumbe kuna waamuzi wanachagnia kuzifanya timu zifike kusikostahili, hivyo ni wakati sasa kwa TFF na TPLB kuchukua hatua haraka ili kuwa fundisho kwa waamuzi wengine kama hao wenye nia ovu ya kufifisha juhudi za serikali kuhakikisha soka la nchi hii linakua zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Elizabeth Zaya

## Muungwana Lazima Nilonge

# Malengo ya Rais Samia kuanzisha Tamasha la Utamaduni yazingatiwe

**MICHEZO** ya riadha, baiskeli, kushindana kula na kunywa vinywaji vya asili, mashindano ya soka, maonesho ya kibiashara ya magari ya zamani, pamoja na mashindano ya ngoma za asili yanatarajia kulipamba Tamasha la Kitaifa la Utamaduni linalotarajiwa kufanyika mkoani Ruvuma kuanzia Septemba 20 hadi 23, mwaka huu.

Tamasha hilo litafunguliwa na Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro na mgeni rasmi katika kilele chake anatarajiwa kuwa Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kwa mujibu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ndio waratibu wa tamasha hilo, mwaka huu linatarajiwa kuwa na vionjo mahsusi ikiwamo mirindimo ya kiasili kuanzia mavazi, maonesho, visasili na visakale.

Maonesho mengine yanayotarajiwa katika tamasha hilo ni pamoja na onesho maalumu la matumizi ya kanga ikiwa ni vazi la utamaduni wa Mtanzania na kutakuwa na kliniki itakayohusu sekta hiyo ya utamaduni na litakuwa na zaidi ya vikundi 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Tamasha hilo ni njia mahsusi ya kukuza viwanda vya ubunifu na linaandaliwa katika namna ya kuzingatia tunu za taifa pamoja na vivutio vya kiutamaduni.

Wakati tamasha hilo linafanyika mkoani humo, ikumbukwe kuwa mkoa huo wa Ruvuma ni miongoni mwa maeneo machache hapa nchini ambayo yana hazina kubwa ya utajiri wa kihistoria na kishujaa.

Mkoa huo pia umejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii wa kiutamaduni na kupitia tamasha hilo ambalo serikali mwaka huu imeamua kulipeleka huko kama utekelezaji wa agizo la Rais Samia la kutaka matamasha hayo kufanyika kwa mzunguko kila mkoa, lengo likiwa ni Watanzania wajue mila na desturi za kila mkoa na kuwa na mashindano ya ngoma za asili na washindi kupewe tuzo, linatarajiwa kuhudhuriwa na wageni kutoka maeneo mbalimbali.

Kupitia tamasha hilo, kuna haja kwa viongozi na watalaamu katika sekta hiyo ya utamaduni na michezo, kuongeza nguvu ya uhamasishaji kwa wananchi na wadau kutoka katika sekta mbalimbali kutumia tamasha hilo kama sehemu ya kujifunza asili na tamaduni zao na kuzitumia kutangaza utalii wa kiutamaduni katika maeneo wanakotoka.

Yaani kila mkoa utumie tamasha hilo kujifunza na kisha kwenda kuendeleza matamasha mengine ya namna hiyo katika mikoa yao kwa kutumia tamaduni zao, kama fursa ya kuwavutia watalii kama sehemu ya utalii wa kiutamaduni ili wanufaike kwa kujipatia kipato na kujiletea maendeleo binafsi, kwenye maeneo yao na hata taifa kwa ujumla.

Ikumbukwe kwamba wakati Rais Samia anaagiza kuanzishwa kwa tamasha hilo, alitaka pamoja na kuwakumbusha kuenzi tamaduni zao, lakini litumike kujinufaisha kiuchumi.

Alitaka litumike katika manufaa kwa kulifungamanisha na fursa za kiuchumi, kutangaza utalii na utamaduni wa Kitanzania katika mataifa mbalimbali na kuinua biashara, michezo na ubunifu kwa ujumla.

Nyingine alitaka litumike kuonesha utamaduni wa Mtanzania kama msukumo madhubuti wa utangamano wa kitaifa kwa kuwaleta na kuwaunganisha pamoja wadau, viongozi wa sekta mbalimbali, wananchi kama sehemu ya kuendelea kuenzi urithi wa utamaduni wa Mtanzania.

Kwa mfano miongoni mwa mambo ambayo yanatarajiwa kupambana katika tamasha hilo la Kitaifa mkoani Ruvuma ni pamoja na utamadudi wa vazi la Kanga ambalo karibu kila mkoa hapa nchini unalitumia, vyakula navyo karibu kila mkoa unavyo vyake, kwa hiyo vinaweza kutumika kama fursa kwa kila mkoa kuwa na utaratibu wa kubadilisha tamaduni zao hizo kwa kutoka mazoea ya kawaida na kuziwekea utaratibu mzuri ambao utakuwa ni fursa ya utalii wa kiutamaduni na kuwaingizia kipato.

Kama hili litafanyika kila mkoa hata kabla ya kusubiri kufikiwa na tamasha la Kitaifa la Utamaduni, itasaidia kuleta mwamko mkubwa kwa jamii kutumia tamaduni zao kama fursa na hata kujijengea utaratibu wa kutembeleana kujifunza na kujionea kwa mkoa mwingine, lakini pia kuvutia watalii kutoka mataifa mengine ambayo yote hiyo itakuwa inaingiza kipato.

# DC atoa wiki tatu walimu wahamie kijijini

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

MKUU wa Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, Suleiman Mwenda, ametoa wiki tatu kwa walimu saba wa Shule ya Msingi Kisana, Kata ya Kisiriri kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua kutokana na kuishi nje ya kituo chao cha kazi wakati shule hiyo ina nyumba za kutosha kwa ajili ya yao.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero ambapo walimweleza kuwa walimu saba kati ya wanane wa shule hiyo wanaishi mjini Kiomboi, makao makuu ya wilaya.

Wananchi hao walisema wanashangazwa na kitendo cha walimu wa shule hiyo kutoishi katika kituo chao cha kazi ilhali nyumba za walimu zipo; wanasafiri umbali wa zaidi ya kilometa 16 kila siku kutoka mjini Kiomboi hadi kijijini huko kutekeleza majukumu yao.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Mwenda alisema kuwa katika kikao kilichofanyika ukumbi wa halmashauri, alitoa maelekezo kwamba watumishi wote waishi katika vituo vyao vya kazi, hivyo inashangaza kuona walimu hao hawajatekeleza agizo lake.

"Ninatoa wiki tatu kwanza waandike maelezo kwanini wanaishi mbali na vituo vyao vya kazi na pili wahame haraka na kama yupo ambaye hayuko tayari kuishi kijijini, aandike barua ya kuacha kazi, tutamtafuta ambaye anataka kazi," aliagiza Mwenda.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Madata Simba, alisema shule hiyo ina walimu wanane, lakini anayeishi kijiji huko ni yeye pekee huku wengine wakiishi mjini Kiomboi.

Alisema ni kweli nyumba kwa ajili ya walimu hao zipo, lakini hakuna vyoo bora, hali ambayo imewafanya walimu hao washindwe kuishi kijijini huko.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Mwenda alimwuliza Mtendaji wa Kijiji cha Kisana, Lucy Chawake, kama anafahamu changamoto ya nyumba hizo kutokuwa na vyoo bora; naye alimjibu kuwa hajapewa taarifa.

Mwenda alisema hata kama nyumba hizo hazina vyoo bora, wananchi hawawezi kuvifanyia ukarabati kwa sababu walimu hawataki kuishi huko.

Aliahidi kutoa mabati 20 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa vyoo hivyo na kuwataka wananchi washiriki ujenzi, ili walimu hao waache kisingizio cha ukosefu wa vyoo.



Washiriki wa mafunzo ya watendaji wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mkoani Singida wakifanya majaribio kwa vitendo ya uboreshaji wa taarifa za mpigakura kwa kutumia mashine za BVR wakati wa mafunzo ya siku mbili ya watendaji wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mkoani Singida jana. Mkoa wa Singida na Dodoma wanatarajia kuanza uboreshaji Septemba 25 hadi Oktoba mosi mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Zitto Kabwe ataka kasi utekelezaji mradi wa Mchuchuma na Liganga

**Na Halfani Chusi**

KIONGOZI mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema kitendo cha serikali kusuasua kukamilisha mradi wa Mchuchuma na Liganga, kinawakosesha vijana ajira.

Zitto aliyasema hayo jana akiwa katika mwendelezo wa ziara ya viongozi wa chama hicho wilayani Ludewa, mkoani Njombe, baada ya kubaini hakuna kinachoendelea katika mradi huo.

Alisema alikuwa anasikia mradi huo unapigiwa kelele na wabunge wa zamani na hata alipoingia bungeni alifanya hivyo, lakini hakuna kilichobadilika.

Alisema katika kuhakikisha hilo linatimia, kipindi cha nyuma yeye na aliyekuwa Mbunge wa Ludewa, Deo Filikunjombe walipambana wakatafuta mwekezaji, lakini hakufanikiwa kutokana na kile alichokiita "konakona za serikali".

Zitto alisema alishangaa kuona serikali inafurahia kulipa fidia ya Sh. bilioni 15 kwa wakazi kupisha eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji wakati ilipaswa ifanye hivyo tangu miaka 10 iliyopita.

Alisema nchi inapoteza fedha nyingi kuagiza chuma nje ya nchi wakati ina utajiri wa chuma Ludewa.

"Na Mwenyezi Mungu anavyotupenda, pembeni yake akaweka makaa ya mawe ambayo yanatumika kuyeyusha chuma ili kupata chuma cha pua, lakini miaka yote hakuna kilichofanyika.

"Tunajenga reli tunajisifia, tunanunua chuma kutoka China, maana yake tumepeleka ajira China wakati vijana wetu wako mtaani wanahangaika na ajira," alilalama.

Alikumbushia kwamba mwaka jana alipokuwa Makambako, alihoji sababu za serikali kupata kigugumizi kutekeleza mradi huo.

Alisisitiza kuwa ili kutengeneza msingi wa uchumi wa viwanda, lazima tuwekeze katika chuma akisisitiza hakuna uchumi wa viwanda bila bidhaa hiyo.

"Kitu cha ajabu leo ninaambiwa na viongozi eti kiwanda cha kuongeza thamani kwenye chuma kitajengwa Makambako! Kwa hiyo, malighafi itatoka Ludewa kwenda huko? Uchumi wa wapi huu? Akili za kipuuzi kabisa.

"Chuma ni 'madude' makubwa, unayapelekaje huko kabla hayajapungua uzito hapa Ludewa? Serikali iseme imebadilisha lini sera yake ya ujenzi wa reli kutoka Mtwara, Mbamba Bay mpaka Ludewa kwenye Mchuchuma na Liganga," Zitto alisema kwa ukali.

Alikosoa kitendo cha serikali kuendelea na mpango wa kujenga Kiwanda cha Chuma Makambako, akisisitiza si uamuzi mzuri; baadala yake kijengwe Ludewa.

Katika hatua nyingine, Zitto alisema chama chao kinatoa siku 14 kwa uongozi wa Mkoa wa Njombe kuweka jiwe la ujenzi wa Shule ya Sekondari Ruhuhu, akisisitiza isipofanya hivyo chama chake kitachangia mifuko 600 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Zitto alitoa kauli hiyo baada ya kupewa taarifa kuwa ujenzi wa shule hiyo licha ya kwamba tayari wanakijiji walishafyatua matofali 100,000 na kukusanya mawe kwa ajili ya kuanzisha ujenzi, lakini hakuna kilichofanyika.

"Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakitaki Sekondari ya Kata Ruhuhu ijengwe, sisi tutajenga nimeambiwa mmeshafyatua matofali 100,000, mmekusanya mawe mmeanza kusomba mawe kupeleka eneo la shule.

"Mimi sina kazi walininyang'anya ubunge, nipo tu mtaani, kazi yangu ni kutetea haki, kuwajengea ukombozi wa fikra. Lakini mimi sina utajiri wa mali wala fedha, lakini nina marafiki matajiri.

"Na marafiki zangu wote wananisikia, ninataka niwaambie popote duniani walipo leo nipo Ruhuhu watoto wanatembea kilomita 20 kufuata masomo ya sekondari kata jirani ya Manda," alisema Zitto.

Aliahidi kuwa kwa niaba ya marafiki zake, kuanzia jana watakuwa na harambee ya kukusanya mchango, ndani ya wiki moja watapeleka mifuko ya saruji 600 ili shule ianze kujengwa.

"Diwani mwambie Mkurugenzi Mtendaji na Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa nitamwambia mimi mwenyewe, ninajua pa kukutana naye, asipoweka jiwe la msingi ndani ya siku 14, zijazo tutamtuma kiongozi wetu wa chama tutakuja hapa na mifuko 600 ya saruji na tutaweka jiwe la msingi sisi wenyewe na ujenzi utaanza," alisema Zitto huku akishangiliwa na wananchi hao.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# WRIFOM yawezesha waandishi kuandika habari za demokrasia

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Waandishi wa Habari Wanawake (WRIFOM) limezindua rasmi programu ya kuwawezesha waandishi wa habari wa kike kuandika habari za kuibua wanawake waliofanya vizuri kwenye demokrasia nchini lakini hawajatambuliwa ipasavyo.

Programu hiyo ilizinduliwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya mstaafu, Betty Mkwasa ambaye pamoja na mambo mengine, aliwataka waandishi hao waliochaguliwa katika mradi huo, kufanya kazi kwa ubunifu kuwaibua wanawake waliofanya mambo mazuri kwenye eneo hilo la demokrasia na kuacha alama ili watumike kama mabalozi kwa wengine.

Alisema wapo wanawake wengi ambao wamefanya mambo makubwa kwenye demokrasia ambao wangeibuliwa, wangechangia kuleta chachu kwa wenzao wanaokata tamaa au kuogopa kufanya shughuli za kidemokrasia kutokana na vikwazo wanavyokutana navyo kutokana na mila na desturi, mfumo dume au mazingira wanayokutana nayo.

"Ninachowaomba, nendeni vijijini mkawaibue wanawake maana wapo baadhi yao ambao hata katika mkutano unaohusu kujadili changamoto zao labda shida ya maji iliyowatesa kwa muda mrefu na wao ndio wanajua uchungu wake, hawasimami kuzungumza hata kama viongozi wa serikali wamekwenda kuwasikiliza, wanasubiri eti mpaka mwanamume ndiye aseme, mama anaambiwa hapaswi kusema.

"Kwa hiyo, wapo baadhi yao hata kama wamefanya mambo mazuri wanaogopa kutoka na kuzungumza kwa sababu ya kuogopa hizo mila kwenye jamii zao, hivyo ninategemea kwamba ninyi waandishi wa habari mtafanya kazi nzuri ya kuwaibua wanawake hao.

"Ninawaomba ndugu zangu ninyi waandishi wa habari, unapofanya jambo lolote lile unatakiwa ujitahidi uache alama, usifanye kitu kwa sababu kinafanyika, jitahidi kila unavyoweza na ninaamini mnapokwenda kufanya kazi hii mtaliangalia hilo, mkumbuke kwamba jamii inawahitaji na inawategemea," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya waanzilishi wa WRIFOM, Chelu Matuzya, alisema lengo la mradi huo ni kuunga mkono harakati za wanawake kwenye demokrasia na kuondoa mitazamo hasi katika jamii.

"Ipo mitazamo hasi kwamba wanawake hawawezi kwenye siasa, ukiwapa nafasi hawawezi kufanya vizuri, ipo mingi tunaifahamu lakini lengo la kufanya huu mradi ni kwa sababu tunaamini kwamba habari tutakazoandika zitaleta mabadiliko makubwa.

"Lakini pia zitasaidia kuonesha uwezo wa wanawake kupitia mambo ambayo wameyafanya na hivyo kubadili mitazamo hasi iliyopo katika jamii na kuongeza motisha kwa wanawake hao na wale ambao wanatarajia au kutamani kuingia katika nyanja hiyo," alihimiza.

Chelu alisema changamoto nyingi ambazo baadhi ya wanawake wamekuwa wanapitia hususani wanapoingia katika demokrasia, zimechangia waone kwamba siasa au mambo ya kidemokrasia hayana maana na kwamba habari za kuwaibua ambazo zitaandikwa na waandishi wa habari zitasaidia kuwatia moyo na hata kuleta usawa wa kidemokrasia.

Alisema wameamua kuja na mradi huo kwa sasa kwa sababu wanatambua kuwa hakuna demokrasia kamili bila mchango wa mwanamke.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Dastan Kamanzi, alisema wapo wanawake wengi ambao wanafanya kazi kubwa katika maeneo yao kama ilivyo kwa wanaume, lakini mchango wao haujathaminiwa au kutambuliwa sana.

"Kwa mfano, katika baadhi ya uchaguzi, wapo wanawake walijitokeza kugombea nafasi za juu kabisa, tena wengine zilikuwa kwenye nafasi ya urais wakishindana na wanaume, lakini pamoja na uthubutu huo hawakupewa nafasi kubwa kwenye vyombo vya habari.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara Incubator wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kai Mollel (kushoto), akizungumza kwenye kongamano la Wiki ya Asasi za Kiraia (CSO week 2024) lililofanyika jijini Arusha wakati wa mjadala wa 'Nafasi na Umuhimu wa Uwekezaji wa Fedha katika Ukuaji Uchumi wa Tanzania na Afrika'. Kulia ni mwakilishi kutoka UTT, Hilda Lyimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji kokoto wapatiwa vifaa

**Na Frank Monyo**

WAJASIRIAMALI wadogo 500 wanaojihusisha na uchimbaji na uchakataji kokoto jijini Dar es Salaam, wamewezeshwa vifaa kinga na kupatiwa mafunzo ya usalama na afya kwa ajili ya kuwaepusha na ajali, magonjwa na vifo vinavyosababishwa na vihatarishi vilivyoko katika mazingira ya kazi.

Uwezeshaji huo umefanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ikiwa ni utekelezaji wa jukumu lake la msingi la kujenga uelewa wa masuala ya usalama na afya miongoni mwa waajiri, wafanyakazi na wananchi kwa ujumla.

Makundi yaliyonufaika na uwezeshaji huo kwa hatua ya awali ni wale ambao wanafanya shughuli zao katika maeneo ya Boko Magereza, Kata ya Bunju, Wilaya ya Kinondoni na maeneo ya Mjimwema, wilayani Kigamboni.

Akifungua programu hiyo ya uwezeshaji wachimbaji wadogo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete, alisema pamoja na changamoto zinazowakumba wachimbaji na wachakataji wadogo wa kokoto, yakiwamo matumizi ya teknolojia duni na ukosefu wa mitaji, mchango wa wachimbaji hao katika uzalishaji malighafi za ujenzi ni mkubwa.

"Ninapenda kuwatia moyo kwamba changamoto zilizopo katika sekta hii hazitakuwa za kudumu. Hivyo, niwaombe tushirikiane kuchukua hatua za kuleta mabadiliko chanya katika sekta hii ikiwamo kuhakikisha kwamba shughuli zote zinafanyika katika mazingira salama na tija inaongezeka kupitia matumizi ya teknolojia za kisasa.

"Kwa upande wetu kama serikali, tumeshaanza kuchukua hatua kwa kuanzia na kuwapa elimu kama inavyofanyika leo, lakini tutaendelea na hatua nyingine ikiwamo kutengeneza mazingira wezeshi yatakayopelekea tija kuongezeka kuhakikisha mnapata mitaji kwa ajili ya kununua zana za kisasa ikiwa ni pamoja na kuanzisha shughuli mbadala," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mary Maganga, aliyeshiriki semina iliyokuwa inaendeshwa na wataalamu wa OSHA, alisema kwa kuzingatia mchango wa wajasiriamali wadogo katika maendeleo ya nchi, taasisi yake (OSHA) imeona ni muhimu kuwapa elimu ya usalama na afya wachimbaji hao, ili waweze kuchukua tahadhari dhidi ya ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo yanayotolewa na wataalamu wake kwa wachimbaji wadogo yamejikita katika kuwawezesha kutambua vihatarishi vinavyoambatana na shughuli zao, likiwamo vumbi, joto kali na mtindo wa ufanyaji kazi usiozingatia taratibu za uchimbaji.

Alisema kuwa mafunzo hayo yanaambatana na utoaji vifaa kinga muhimu vilivyogharamiwa na serikali, ili kuwahamasisha wachimbaji hao kuzingatia matumizi sahihi ya vifaa kinga katika kazi zao.

Vifaa kinga vilivyotolewa kwa wajasiriamali hao ni pamoja na barakoa, vikinga mikono (glavu), vizibao vinavyoakisi mwanga (reflective vests) kutambulisha kuwapo mfanyakazi mahali pa kazi pamoja na masunduku ya huduma ya kwanza.

Wajasiriamali walionufaika na uwezeshaji huo, akiwamo Berena Bilal, walishukuru serikali kupitia OSHA kwa uwezeshaji waliopata.

## Kampuni yajivunia kulipa kodi bil. 750/-

**Na Mary Geofrey**

SHILINGI bilioni 750 zimelipwa kama kodi nchini na kampuni, zikigawanywa katika makundi mbalimbali kama vile Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ushuru wa uagizaji bidhaa, kodi ya bidhaa, mishahara na kodi ya mapato.

Uongozi wa SBC Tanzania LTD umesema unajivunia maoni yake yaliyofanya kampuni yao kulipa kiasi hicho na kuwa miongoni mwa walipakodi bora 20 Tanzania, ikirudisha sehemu yake kwa uchumi wa taifa.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni wakati kampuni hiyo ilipoandaa sherehe ya kumuaga kwa heshima Mkurugenzi Mtendaji anayestaafu, Avinash Jha.

Ziad El Khalil, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, alimkabidhi Avinash Tuzo ya Mwenyekiti ya Heshima na Ubora 'The Chairmans Award of Honor & Excellence'.

Katika hotuba yake, El Khalil alisema kuwa wameongeza idadi ya wafanyakazi wao kwa karibu mara tatu kutoka wafanyakazi 545 wa familia ya muda mrefu mnamo mwaka 2001 hadi wafanyakazi 1,350 mnamo 2024, na wafanyakazi wa muda mfupi kutoka 350 mnamo 2001 hadi karibu 1,500 mwaka huu.

"Lakini muhimu zaidi, tumeunda maelfu ya fursa za kibiashara kwa watu binafsi na kampuni ndogo na za kati kufanya biashara na bidhaa zetu kote Tanzania," alisema.

El Khalil alitoa shukrani kwa Serikali ya Tanzania na wananchi, akisema "Tanzania imekuwa mwenyeji wa kujivua kwa kampuni yetu na sekta nzima ya biashara, ikitoa mazingira rafiki kwa biashara ambayo yameiruhusu kampuni kama yetu kustawi.

"Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi umekuwa mfano wa mafanikio. Ushirikiano huu haujawahi kuwa imara zaidi kuliko ilivyo sasa chini ya utawala wa sasa unaoongozwa na Rais Mama Samia Suluhu Hassan.

"Ajenda yake ya kuimarisha biashara na Falsafa yake ya R4 (Maridhiano, Uvumilivu, Mageuzi na Kujenga Upya) - imeenda mbali sana katika kuibadilisha Tanzania kuwa nguvu ya kiuchumi na mahali pa kuchagua na wawekezaji.

"Tunashukuru kwa msaada na ushirikiano ambao umetolewa kwetu kwa miaka mingi na Serikali ya Tanzania na taasisi zake zote za kiserikali," alisema.

El Khalil alisema uhusiano wa Avinash na kampuni yao ulianza mnamo Januari 2001, akiitaja ni safari iliyojawa na kujitolea, bidii na dhamira thabiti kwenye ubora.

Alianzia cheo cha Meneja wa Kiwanda mjini Arusha mwaka 2001 hadi kupanda kwake kuwa Msimamizi wa Fedha Dar es Salaam mwaka 2003, kisha kuwa Ofisa Mkuu wa Fedha mnamo mwaka 2006, na hatimaye kuwa Mkurugenzi Mtendaji mnamo mwaka 2014 na baadaye kualikwa kujiunga na Bodi ya kampuni yao mnamo mwaka 2015.

Alisema kuwa Avinash amekuwa nguvu ya kuendesha mafanikio ya kampuni hiyo ambayo imeongeza kiasi cha mauzo ya mwaka 2001 mara 25 katika miaka 23.

## Wanaharakati Marekani kusaidia wagonjwa selimundu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAHARAKATI 20 raia wa Marekani, wamewasili nchini kwa ajili ya kuchagiza kampeni maalumu ya kuchangisha fedha za kusaidia waathirika wa ugonjwa wa selimundu, unaohusisha kurithi vinasaba kutoka kwa wazazi.

Kwa mujibu wa kanzidata ya Wizara ya Afya, inaonyesha watu 200,000 nchini wana ugonjwa wa selimundu, huku watoto 11,000 huzaliwa wakiwa na ugonjwa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Sickle Forward la Marekani, Dk. Allan Anderson, alisema jana jijini Arusha kwamba watapanda Mlima Kilimanjaro, ili kukusanya fedha zitakazotolewa kwa ajili ya watu wanaosumbuliwa na ugonjwa huo katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Tunalenga kuongeza utambuzi wa haraka wa watoto wachanga ili kuanza matibabu mapema katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Huu ni mwezi wa uhamasishaji na tunashirikiana na Serikali ya Tanzania na wadau wengine wa afya," alisema Dk. Allan.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wanaguswa zaidi na umuhimu wa kusaidia vitendanishi, kwa ajili ya upimaji wa ugonjwa huo, ili kuokoa vifo vya watoto wadogo vitokanavyo na ugonjwa huo.

Alisema hadi sasa, wameshakusanya zaidi ya Dola za Marekani milioni 1.2 kwa ajili ya kuzisaidia nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Lengo letu ni kusaidia uchunguzi na matibabu katika maeneo ya nchi hizo pamoja na nyingine na tunafanya kazi na nchi za Afrika Magharibi pia ikiwamo Mali, Togo, Gabon," alifafanua.

Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza Mkoa wa Arusha, Dk. Edna Ntulwe, alisema elimu ni muhimu kuendelea kutolewa ili kukata mnyororo wa kuzaliwa watoto wenye selimundu.

Naye Mtendaji Mkuu wa Asasi ya Mwamvuli ya Wadau wanaofanya kazi kwenye ugonjwa huo, Dk. Deogratias Matanda, alisema tatizo la selimundu nchini bado ni kubwa nchini.

"Kati ya watoto zaidi ya 10,000 wanaozaliwa na tatizo hilo kati yao tusipotambua mapema na kuanza matibabu, asilimia 70 hadi 90 hufariki kabla ya kufika umri wa miaka mtano," alisema.

Mwanaharakati na shujaa wa selimundu, anayepambana kutoa elimu juu ya ugonjwa huo, Sanyu Senga, alisema kutokana na kukosekana kwa elimu ya ugonjwa wa selimundu, baadhi ya wazazi wa watoto wenye ugonjwa huo wamekuwa na imani potofu na kuwapeleka watoto wao kwa waganga wa kienyeji, badala ya hospitali.

Hivyo, aliiomba serikali na wadau wa afya nchini kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya ugonjwa huo na kuongeza uelewa ili kuepusha vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vitokanavyo na kukosa matibabu.

# Mjumbe usalama wa chakula akoshwa na utendaji wa WVC

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

NAIBU Mjumbe Maalum wa Usalama wa Chakula Duniani wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Anna Nelson, amefurahishwa na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Uhifadhi wa Mbegu (WVC), kinavyosadifu maono na dira ya Kituo cha Chakula Ulimwengu, ambacho kimezindua mpango wake mpya wa uokoaji wa baioanuwai Afrika.

Amesema USAID na washirika wa karibu wa AGRA katika mpango wa dira ya mazao na udongo uliobadilishwa, wanalenga kujenga ustahimilivu, kujenga mifumo ya chakula inayostahimili mabadiliko ya hali ya hewa yenye lishe na aina mbalimbali za mazao zinazokuzwa katika udongo wenye afya.

Alieleza hayo jana baada ya kutembelea kituo hicho kilichoko Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, kujifunza kuhusu kazi muhimu wanayofanya ili kuongeza ustahimilivu wa mifumo ya chakula.

"Wanachofanya hapa kuhifadhi na kutumia baioanuwai ya kilimo tuliyonayo ni muhimu sana katika mabadiliko ya hali ya hewa yetu. Nimefurahi sana kusikia juu ya kazi nzuri wanayofanya kupata chaguzi zaidi, aina nyingi za mazao, aina nyingi za mazao zinazostahimili ukame. Kwa mfano aina za mazao zenye lishe kwa wakulima wetu wote, tena wa hapa Tanzania na duniani kote," alisema.

Aliongeza: "Kwa hiyo imekuwa ni furaha kubwa na inatia moyo sana kuona wanachofanya hapa Tanzania. Hakika, inatia moyo pia kwamba kituo cha mboga duniani kinafanya kazi kwa karibu sana, bila shaka na Serikali ya Marekani, ambayo tunajivunia".

Mkurugenzi wa AGRA, Vianey Rweyendela, ambaye aliambatana na wageni hao alisema kwa sasa Tanzania haina uhaba wa chakula bali ina uhaba wa chakula chenye lishe bora.

Mkurugenzi wa World Vegetable Center Tanzania, Coletha Ndunguru, alisema kwa sasa wamelenga kukuza zaidi uelewa wa jamii na dunia kwa ujumla kuhusu mboga za asili za Afrika.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, Amiri Sheiza, akimkabidhi kishikwambi mmoja wa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli kupitia vyanzo vya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2023/24, imenunua kompyuta 42 zenye thamani ya Sh.milioni 10.5. **PICHA: CHEJI BAKARI**

# Kata sita zafikiwa elimu unyanyasaji kingono

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

AJENDA ya kumaliza masuala ya unyanyasaji wa kingono, unyonyaji wa kiuchumi na kukuza wanawake katika nafasi za uongozi imeanza kufikishwa katika kata sita zilizokithiri matukio hayo.

Kata hizo ni Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi) na Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

Kwa mujibu wa Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaolenga kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Veronica Ollomi, pia mradi huo utashughulikia uimarishaji haki za kifeminia na haki za kijamii. Mradi huo wa miezi sita, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT).

"Lakini kutoa ujuzi wa utetezi kwa wanaharakati katika suala zima la kupinga ukatili wa kijinsia ili kukabiliana na mila na mifumo ambayo inasababisha kutokuwa na usawa wa kijinsia katika Mkoa wa Kilimanjaro," alisema na kuongeza:

"Tutaongeza uelewa wa jamii kuhusiana na masuala ya sheria, masuala ya ukatili wa kijinsia na mbinu za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ambayo tutayafanyia kazi.

...Tunajua katika mchakato kama uchaguzi kuna rushwa ya ngono na rushwa tofauti. Je, yeye kama mwanamke anayetamani kuwa kiongozi akabiliane vipi na hizo changamoto ambazo zinaweza zikajitokeza katika mchakato mzima wa kugombea hizo nafasi za uongozi."

Mratibu huyo, amefafanua zaidi kwamba, idadi ambayo itafikiwa katika kata zote sita, ni watu 100 katika kuwajengea uwezo lakini katika hao, 72 ni wanawake na 28 ni wanaume.

Alisema: "Tutaendesha midahalo katika ngazi ya jamii kuhusu masuala ya ukatili, kujadili masuala muhimu ya ushirikishwaji wa wanawake katika masuala ya uongozi."





# Watano kizimbani tuhuma wizi vifaa vya umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU watano wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kahama kwa tuhuma za wizi wa nyaya za umeme zenye thamani ya Sh. milioni 54.

Nyaya hizo zilikuwa zinatarajia kutumika katika mradi wa usambazaji wa nishati ya umeme vijijini Kata ya Idahina, Halmashauri ya Ushetu.

Akisoma mashtaka hayo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Jukaeli Jairo, aliiambia mahakama kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo Septemba 3, mwaka huu katika miji ya Kahama na Dar es Salaam, kwamba walikutwa na bando tatu za nyaya ya aluminum.

Jairo alidai watu hao wanakabiliwa na makosa mawili ambayo ni kuunda genge la kuharibu kwa makusudi mali za umma kinyume na Sheria 4(1)(a) ikisomwa pamoja na 57(1) na 60(2) ya Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Kosa la pili likiwa ni wizi wa vifaa vya umma kinyume na kifungu cha Sheria Namba 258(1)(2)(a) na 265 ya Kanuni ya Adhabu Sura 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Aliiwataja watu hao kuwa ni Erick Rweyemamu (36) mkazi wa Missenyi ambaye ni fundi umeme, Kaijage Kagenyi (27) mkazi wa Katoro na Carlos Chamanga (29) ambaye ni fundi umeme na mkazi wa Mlimba.

Wengine ni Ngwea Sufian (29) fundi umeme na mkazi wa Sinai mkoani Dodoma, Lemi Mtwale(34) mkandarasi na mkazi wa jijini Dar es Salaam na Rotan Nzowa (38) fundi umeme na mkazi wa Kahama.

Kesi hiyo namba 26208/2024 ilisikilizwa na Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Kahama, Edmund Kente na nyaya za umeme zilizoibiwa zilikuwa ni mali ya Kampuni ya Iddcon Investment Limited.

Licha ya kusomewa mashtaka hayo, watuhumiwa wote hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na kuwa moja katika ya mashtaka yanayowakabili ni la uhujumu uchumi, kwamba mahakama hiyo haina uwezo kisheria wa kulisikiliza.

Hata hivyo watuhumiwa hao waliiomba mahakama hiyo kupewa dhamana dhidi yao, ombi ambalo halikupokelewa kutokana na Hakimu Kente kuwaeleza kuwa hajapata kibali cha kufanya hivyo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 27, mwaka huu itakapoitwa tena.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya mahakama, Mkurugenzi wa Kampuni ya Iddcon Investment Limited, Iman Matabula alisema mpaka sasa wameshapata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 400 kutokana na wizi wa vifaa mbalimbali.

Mtubula alisema ili kutokomeza wizi huo kwenye miradi ya serikali ni vema wanunuzi nao wakakamatwa kwa sababu wao ndiyo wanaohamasisha vijana kuiba na kwenda kuwauzia.



Ofisa Sheria kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), George Msaki (kushoto), akitoa elimu na huduma ya usajili wa biashara pamoja na majina ya biashara kwa mmoja wa wafanyabiashara waliofika katika banda la wakala huo lililoko katika Maonesho ya 19 ya Biashara Afrika Mashariki yanayofanyika jijini Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Akutwa amefariki dunia kando ya mto

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Kyoruba wilayani Tarime mkoani Mara, Elia Sigirya, amekutwa amefariki dunia kando ya Mto Renyamabi, huku mwili wake ukiwa na jeraha ubavuni.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Tarime/Rorya, Michael Njera, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa jeshi hilo linaendelea na msako kuwabaini wahusika wa tukio hilo.

Akisimulia tukio hilo baba mzazi wa kijana huyo, Sigirya Mwita, alisema mtoto wake alifikwa na umauti usiku wa Jumatano wakati akirejea nyumbani akitokea Kijiji cha Kebweye.

Alisema mwili wake waliukuta umetupwa kando ya Mto Renyamabi ukiwa na jeraha la kuchomwa na kitu chenye ncha kali ubavuni na kutokwa damu kwa wingi.

Hivyo, aliwaomba wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kusaidia kuwapata wahusika wa tukio hilo, akisema kijana wake alikuwa akimsaidia katika majukumu ya nyumbani kutokana na yeye kuwa mlemavu wa macho.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kyoruba, Ruben Makuri alikiri kutokea kwa tukio hilo na kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano katika kuhakikisha wahusika wa tukio hilo wanakamatwa.

Diwani wa Kata ya Pemba, Seronga Wangwe aliwaomba wananchi kuwa watulivu na kuliachia la Jeshi la Polisi kufanya kazi yao katika operesheni ya kuwasaka waliohusika.

# Bil. 1.4/- kumaliza kero upatikanaji maji Ngara

**Na Judith Julius,** NGARA

NAIBU Waziri wa Maji, Kundo Mathew, amesema Rais Samia Suluhu Hassan amewaelekeza kutenga Sh.bilioni 1.4 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Nyakariba kilichoko Kata ya Kasulo wilayani Ngara.

Kundo alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara yake kijijini humo iliyolenga ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika sekta ya maji pamoja na kusikiliza kero ya maji kutoka kwa wananchi.

Alisema tayari taratibu za utekelezaji wa mradi huo zimeanza, huku akitoa miezi sita mradi huo uwe umekamilika na wananchi waanze kupata huduma ya maji.

Aidha, alimtaka mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha vibarua watakaofanya kazi watoke katika eneo la mradi na siyo wageni kama ilivyozoeleka kwa baadhi ya makandarasi.

Awali kero hiyo iliibuliwa na Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, wakati wa ziara iliyofanywa na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Dk. Emmanuel Nchimbi alipofanya ziara wilayani hapa Agosti.

## Wakimbia makazi wakihofia kukamatwa na polisi

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

WANANCHI katika Kata ya Nguru wilayani Igunga mkoani Tabora wameyakimbia makazi yao wakihofia kukamatwa na Jeshi la Polisi kutokana na kifo cha mkulima Kushoka Kabeya (40).

Kabeya alifariki dunia wiki iliyopita baada ya kushambuliwa na fimbo, mawe na marungu na watu wasiofahamika.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Igunda Kuhenga aliiambia Nipashe kuwa tukio hilo la mauaji lilitokea Septemba, 11, 2024 ambako kundi la wananchi zaidi ya 300 wa kitongoji hicho wanadaiwa kujikusanya na kuanza kumshambulia mkulima huyo.

"Walikuwa wakimtuhumu kuiba ng'ombe mmoja kwa mfugaji ambaye hawakumtaja jina lake ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Bulumbela Kata ya Ziba," alisema Kuhenga.

Alisema licha ya Kabeya (marehemu) kujitetea kutokuhusika na wizi huo wananchi hao waliendelea kumshambulia hadi kumsababishia umauti na baada ya kutekeleza kitendo hicho walikimbia, mwili wa marehemu ulizikwa Septemba 12.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Constantine Mbogambi, alithitibisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa wananchi hao walichukua maamuzi hayo baada ya kumtuhumu kwa wizi.

Kamanda Mbogambi alitoa onyo kwa wananchi ambao wamekuwa na tabia ya kujichukulia sheria mikononi, akiwataka kuacha.

Alisema endapo watabaini kuna wahalifu wanapaswa kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Nipashe
Spotika



HAALAND ... UKURASA 14



RONALDO

# WASHANGILIAJI 10 BORA WA MABAO

**LONDON,** England

KIMSINGI mpira wa miguu unazingatia msisimko, burudani na mabao. Kitu kimoja kinachounganisha nguzo zote tatu pamoja ni sherehe ya mabao.

Katika miaka 40 iliyopita, sherehe za mabao zimekuwa muhimu kwa kufurahia kwetu soka. Kutolewa huko kwa mhemuko, iwe kumechangiwa kwa njia isiyo ya kawaida au kwa mpangilio mzuri, hutoa wakati maalum kwa wale walio ndani ya uwanja na kutazama wakiwa kwenye starehe majumbani mwao.

Hapa tunawaangalia washangiliaji 10 - bora zaidi wa mabao, twende sasa...

**10. Lionel Messi**

Lionel Messi alikuwa akiwatesa mara kwa mara wapinzani wa Barcelona, Real Madrid.

Akiwa ametoka tu kufunga bao la ushindi dakika za lala salama wakati wa ushindi wa 3-2 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, Messi alivua shati lake na kuinua mbele ya umati, jina lake na namba yake ikiwaka kwa waumini wa Madrid wenye hasira.

Lilikuwa bao la 500 la Muargentina huyo na alisherehekea kwa mtindo. Wachezaji wachache wanaweza kufanya sherehe kama hii.

**9. Wayne Rooney**

Mara nyingi ni bora kukumbatia nyakati za aibu zaidi maisha yako, jambo ambalo Wayne Rooney alitolea mfano mwaka 2015.

Baada ya video kuchapishwa ambayo ilionesha kuwa mshambuliaji huyo wa Manchester United alitolewa nje wakati wa mchezo wa ndondi wa kirafiki na uliokolezwa na pombe na mchezaji mwenzake wa zamani Phil Bardsley, Rooney alijibu kwa kusherehekea 'K.O' baada ya kufunga bao dhidi ya Tottenham Hotspur.

**8. Jimmy Bullard**

Jimmy Bullard amejulikana sana na kupendwa kwa ucheshi wake baada ya kustaafu lakini muda wake wa ucheshi ulioneshwa wakati wa mechi na Man City mnamo 2009.

Akiichezea Hull City wakati huo, kiungo huyo na wachezaji wenzake walikuwa wameruhusu mabao manne ya kipindi cha kwanza kwa Man City wakati wa safari ya kwenda Etihad, jambo lililomfanya kocha Phil Brown kutoa mazungumzo ya timu yake ya mapumziko na wachezaji uwanjani mbele ya wafuasi.

Hull wakiwa bado wamepoteza 5-1, Bullard alisherehekea bao lake la kipindi cha pili kwa kuwakalisha chini wachezaji wenzake na kujifanya kuwapa habari nzuri.

**7. Daniel Sturridge**

Daniel Sturridge alijivunia kusherehekea kwake, mara kwa mara alionekana Liverpool wakati mshambuliaji huyo alipokuwa akicheza saini yake ambayo angepunga mikono yake kutoka upande mmoja hadi mwingine.

"Nilikuwa pale na binamu zangu usiku mmoja na nikaanza kucheza ngoma kihalisi bila kitu, nikijidanganya tu. Kisha nikawa kama, 'Hey, nitafanya ngoma hii Jumamosi ikiwa nitafunga!' Ilikuwa ni mzaha, lakini nilifanya hivyo," alisema mshambuliaji huyo.

**6. Robbie Keane**

Mwanasoka asiyethaminiwa sana na sherehe ambayo mara nyingi haikuthaminiwa, kupiga mara kwa mara kwa Robbie Keane.

"Sherehe ilikuwa kitu ambacho nilikuwa nikikifanya nikiwa mtoto. Kama mchezaji, siku zote nilitaka kuwasisimua watu na kuwaburudisha. Ni wazi, kwa kufunga mabao kwanza kabisa, kwa hivyo ndio. Sherehe ilikuja baada ya hapo," alisema.

**5. Peter Crouch**

Peter Crouch ameimarisha nafasi yake katika kitengo cha hazina ya taifa baada ya kustaafu, lakini mara zote alikuwa mwanasoka mwenye tabia ya ajabu uwanjani pia.

Bila shaka, mshambuliaji huyo mahiri alifanana na 'Roboti' na ingawa si mvumbuzi wa hatua hiyo, wote 6'7 waliitekeleza kwa usahihi wa hali ya juu.

Crouch alisherehekea mara kwa mara, kwanza akifanya hivyo dhidi ya Hungary kwa England na aliiokoa kwa matukio maalum - ikiwa ni pamoja na bao lake la 100 la Ligi Kuu ya England 2017.

**4. Mario Balotelli**

Katika moja ya mechi za kukumbukwa zaidi za Ligi Kuu England ni ushindi wa 6-1 wa Man City dhidi ya Man Utd kwenye Uwanja wa Old Trafford mnamo 2011 - mshambuliaji mahiri wa Italia, Mario Balotelli aliandika jina lake kuwa gwiji kwa mabao mawili na kushangilia.

Akiwa ametangulia kufunga dakika ya 22, Balotelli alinyanyua jezi yake ya Man City na kufichua fulana iliyosema: "Kwa nini mara zote ni mimi?"

Kwa upande wa sherehe za mara moja, Ligi Kuu haijaona alama zaidi ya hii, haswa kutokana na ukubwa wa mechi iliyofanyika.

**3. Paul Gascoigne**

"Kulikuwa na takriban tisa kati yetu ambao tulifanya Uenyekiti wa Daktari wa Meno huko Hong Kong, lakini ni wazi, kwa kuwa mimi ni, mimi ndiye niliyepigwa kwa hilo," alisema Paul Gascoigne alipozungumza kuhusu sherehe yake ya Bai kwenye Euro '96.

"Kwa sababu fulani, katika mchezo wa pili dhidi ya Scotland, nilisema tu, 'watu sawa, yeyote anayefunga atakuwa Mwenyekiti wa Daktari wa meno' na kwa bahati nzuri kwangu, ilikuwa mimi."

Hadithi inaeleza kwamba wakati wa ziara ya awali ya England barani Asia, wachezaji kadhaa walifungwa kwenye viti na kujazwa pombe.

**2. Cristiano Ronaldo**

Ikiwa haujaona, kusikia au kufanyiwa sherehe za Cristiano Ronald maarufu 'Siuuu', basi ulikuwa wapi kwa muongo uliopita?

Mmoja wa wachezaji bora kuwahi kucheza mchezo huo na mamilioni ya mashabiki duniani kote, sherehe ya Ronaldo ilishika kasi alipoitumbuiza kwa mara ya kwanza huko Real Madrid. Mreno huyo ambaye hadi leo anatumia sherehe hiyo, alikimbia hadi kwenye bendera ya kona kabla ya kuruka, kugeuka na kupiga kelele 'Siuuu'.

Kwa Kihispania kwa neno 'ndiyo', hali ya kurefushwa na ya ucheshi ya mlipuko wake itadumu milele.

**1. Roger Milla**

Sherehe zimezidi kuwa za kawaida na za kina tangu mwanzoni mwa karne ya 21 na bila shaka ni Roger Milla ambaye tunapaswa kumshukuru kwa jambo hili.

Mcameroon huyo alifanya moja ya sherehe za kwanza mwafaka katika Kombe la Dunia la 1990, akiheshimu mabao yake manne kwenye dimba hilo kwa kucheza kuzunguka bendera ya kona kwa shangwe.

Mchezaji huyo mashuhuri akiwa na umri wa miaka 38, aliisaidia Cameroon kufika robo fainali ya Kombe la Dunia.

## ISIKUPITE

ACHANA na hat-trick aliyofunga juzi dhidi ya Holstein Kiel wakati Bayern Munich ikishinda 6-1, kubwa ni kwamba Harry Kane sasa amefunga dhidi ya klabu zote 18 alizokutana nazo kwenye Bundesliga. Katika historia ya mgawanyiko huo, ni Miroslav Klose pekee ambaye amekutana na wapinzani tofauti zaidi na kufunga dhidi ya wote (28). Lakini Kane sasa amehusika moja kwa moja katika mabao 50 kwenye mechi 35 za Bundesliga akiwa na Bayern tangu kuhama kwake kutoka Tottenham mwaka jana.



## Extra Time

# VIWANJA 10 VIKUBWA ZAIDI VYA SOKA DUNIANI KWA SASA



UWANJA WA RUNGRADO 1ST OF MAY

**LONDON, England**

UKUBWA si kila kitu linapokuja suala la uwanja wa mpira kuwa wa kuvutia, lakini kwa hakika inaweza kusaidia kutoa mazingira ambayo hayawezi kulinganishwa.

Viwanja maarufu zaidi vya soka, bila kujali bara au nchi, mara nyingi hujivunia uwezo wa kubeba idadi kubwa ya mashabiki. Vikiwa vimejazwa kwenye makumi ya maelfu ya mashabiki wenye shauku, viwanja hivi vinaweza kutokeza kelele zenye uwezo wa kupimwa kwa kipimo cha Richter.

Kwa wengine, kusafiri kote ulimwenguni kutazama viwanja hivi na huwa kama hija ya kiroho.

Hapa tunakuletea viwanja vikubwa vinavyochuku mashabiki wengi zaidi duniani kwa sasa...

**10. Uwanja wa Cotton Bowl**
Mahali: Dallas, Marekani
Mashabiki: 92,100

Uwanja wa Cotton Bowl umeandaa mechi nyingi za soka kwa miaka mingi, ukijiita nyumbani kwa Dallas Tornado na Dallas Burn (sasa ni FC Dallas) hapo awali. Kuanzia 2024/25, utakuwa nyumbani kwa timu ya wanawake ya Dallas Trinity kwa msimu wao wa kuanzishwa kwa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake ya Marekani (USL Super League).

Uwanja huo mkubwa wenye uwezo wa kuchukua mashabiki 92,100 uliandaa mechi sita kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 1994, hasa ushindi wa mabao 3-2 kwa Brazil dhidi ya Uholanzi katika robo fainali ya mashindano hayo.

**9. Uwanja wa Rose Bowl**
Mahali: Pasadena, Marekani
Mashabiki: 92,800

California ni nyumbani kwa Rose Bowl, inayojulikana sana kwa kuandaa mchezo wa soka wa chuo kikuu wa Rose Bowl kila Siku ya Mwaka Mpya. Hata hivyo, kwa upande wa soka, inakumbukwa zaidi kwa kuandaa fainali ya Kombe la Dunia 1994 ambapo Roberto Baggio alipiga penalti hiyo juu ya goli.

Pia ulikuwa mwenyeji wa LA Galaxy kwa miaka sita kabla ya kuondoka mwaka wa 2002, huku ukifanyika mara kwa mara kwenye mechi za kirafiki za kujiandaa na msimu mpya kwa baadhi ya timu bora za Ulaya.

**8. Uwanja wa New Administrative Capital**
Mahali: Cairo, Misri
Mashabiki: 93,940

Uwanja mpya kabisa kati ya kumi bora kwa umbali fulani, Uwanja wa New Administrative Capital ulifungua milango yake Januari 2024. Mechi ya kwanza haikuchezwa hadi Machi, huku Misri wakiwakaribisha New Zealand katika Kombe la ACAD la 2024.

Uwanja unabeba watazamaji takriban watu 94,000 ni wa pili kwa ukubwa barani Afrika na unaunda sehemu ya Jiji la Michezo la Olimpiki la Misri huko Cairo. Uwanja unaweza kuwa muhimu katika ofa za siku zijazo kwa hafla kuu za michezo, pamoja na Kombe la Dunia.

**7. Uwanja wa FNB**
Mahali: Johannesburg, Afrika Kusini
Mashabiki: 94,736

Uwanja wa First National Bank Stadium, ambao pia unajulikana kama Soccer City, ndio mkubwa zaidi barani Afrika wenye uwezo wa kuchukua takriban watu 95,000. Ni nyumbani kwa Kaizer Chiefs, moja ya klabu kubwa zaidi Afrika Kusini, na pia ulitumika kwa urahisi kwenye Kombe la Dunia la 2010.

Umeongezeka ukubwa kwa takriban viti 10,000 tangu Kombe la Dunia, ambapo iliandaa fainali kati ya Hispania na Uholanzi. Miaka mitatu baadaye iliandaa fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika kati ya Nigeria na Burkina Faso, na ulikuwa uwanja ambao Nelson Mandela alitoa hotuba yake ya kwanza mjini Johannesburg baada ya kuachiliwa kutoka gerezani mwaka 1990.

**6. Uwanja wa Azteca**
Mahali: Mexico City, Mexico
Mashabiki: 95,500

Estadio Azteca ni mojawapo ya viwanja vya soka maarufu katika soka duniani na ni nyumbani kwa Klabu ya Mexico Club America, pamoja na Timu ya Taifa ya Mexico.

Ulikuwa uwanja wa kwanza kufanya fainali mbili za Kombe la Dunia, na ya kwanza ilifanyika 1970 wakati Brazil ilipoifunga Italia 4-1. Ya pili ilikuja miaka 16 baadaye huku Diego Maradona akiipaisha Argentina kupata utukufu, na uwanja huo ukaandaa robo-fainali ambayo ilishuhudia Wamarekani wa Kusini hao wakifunga bao maarufu la 'Mkono wa Mungu' dhidi ya Uingereza.

Uwanja huo pia utaandaa mechi katika Kombe la Dunia la 2026.

**5. Uwanja wa Camp Nou**
Mahali: Barcelona, Hispania
Mashabiki: 99,354

Timu ya wanaume ya Barcelona kwa sasa inacheza mechi zao za nyumbani katika Uwanja wa Lluis huku Camp Nou ukifanyiwa ukarabati na 'La Blaugrana' watatamani kurejea kwenye nyumba yao kubwa haraka iwezekanavyo.

Uwanja wa Barcelona walionyakua ushindi wa ajabu tangu 1957, ulikuwa mwenyeji wa wababe hao wa Katalunya baada ya kuondoka kwenye nyumba yao ya awali ya Camp de Les Corts. Bado ndio uwanja mkubwa zaidi nchini Hispania na Ulaya, unaochukua watazamaji chini ya 100,000 kwenye kilele chake.

Katika hali isiyo ya kawaida, michezo mitano kwenye Kombe la Dunia ya 1982 ilichezwa Camp Nou, ikiwa ni pamoja na nusu fainali kati ya Poland na Italia.

**4. Uwanja wa Melbourne Cricket Ground**
Mahali: Melbourne, Australia
Uwezo: 100,024

Melbourne Cricket Ground, kama jina linavyopendekeza, huwa mwenyeji wa Kriketi nyingi, huku pia ikiandaa mechi za soka za Australia, muungano wa raga na Ligi ya Raga.

Umekuwa uwanja unaotumiwa na Timu ya Taifa ya Wanaume ya Australia, mara nyingi huko nyuma, huku watalii wa Ulaya wakifanya mechi za kirafiki huko mbele ya umati wa watu. Mechi ya kirafiki ya Newcastle United na Tottenham Hotspur baada ya msimu mpya Mei 2024 ilichezwa hapo.

Mechi kadhaa katika Olimpiki ya Majira ya joto ya 2032 zimepangwa kuchezwa katika uwanja wa kuchukua watu 100,024.

**3. Uwanja wa Ohio**
Mahali: Columbus, Marekani
Mashabiki: 102,780

Tukirudi Marekani, tuna Uwanja wa Ohio mjini Columbus. Kwa sasa unatumiwa na timu ya chuo cha mpira wa miguu cha Ohio State Buckeyes, lakini hapo awali ilikuwa nyumba ya wachezaji wa Ligi Kuu ya Soka Columbus Crew kati ya 1996 na 1998.

Mechi ya ufunguzi ya Columbus Crew kwenye ukumbi ilivutia zaidi ya mashabiki 25,000 na klabu iliondoka uwanjani wakati Uwanja wa Columbus Crew ulipojengwa mnamo 1999.

Ushindi wa Manchester City wa 4-2 dhidi ya Chelsea wakati wa maandalizi ya msimu wa 2024/25 uliandaliwa kwenye Uwanja wa Ohio, huku Erling Haaland akiongeza hat-trick nyingine kwenye jumla yake.

**2. Uwanja wa Michigan**
Mahali: Ann Arbor, Marekani
Mashabiki: 107,601

Uwanja wa Michigan ni mkubwa. Ndio uwanja mkubwa zaidi nchini Marekani na wa tatu kwa ukubwa wa maelezo yoyote duniani. Una uwezo wa ajabu wa karibu watu 108,000, na umati wa watu umefikia 115,000 hapo awali.

Kwa hakika, umati wa rekodi ya Marekani kwa mechi ya soka ulikuja kwenye Uwanja wa Michigan wakati mechi ya kirafiki kati ya Real Madrid na Manchester United ilishuhudia watu 109,318 wakiketi katika viti vyao.

Michigan Wolverines hucheza kandanda ya vyuo vikuu vya Amerika kwenye uwanja huo na imekuwa ikitumika kwa kiwango kidogo tu kuandaa mechi za kandanda hapo awali. Pia huwa mwenyeji wa michezo ya mara kwa mara ya hoki ya barafu.

**1. Uwanja wa Rungrado 1st of May**
Mahali: Pyongyang, Korea Kaskazini
Mashabiki: 114,000

Uwanja wa madhumuni mengi huko Pyongyang, Korea Kaskazini, Uwanja wa Rungrado 1st wa Mei ulifunguliwa mnamo 1989 na sasa unaweza kuwa na idadi ya watu 114,000. Ingawa unatumika kuandaa hafla mbalimbali za michezo, pia umetumika kama uwanja wa hotuba za kisiasa kwa hadhira kubwa.

Timu za Taifa za Wanaume na Wanawake za Korea Kaskazini zinautumia uwanja huo nyumbani kwao, lakini pia uliandaa maonyesho makubwa zaidi ya michezo ya viungo na mieleka kuwahi kutokea duniani.

Kuna madai kwamba uwanja huo bado unaweza kupanuliwa ili kutoshea watu 150,000.

## Nukuu


"Nilitaka sana kurudi, nilikuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu, kidogo kidogo nilikuwa nikifanya mazoezi na kundi, nikiwa najisikia vizuri na ndiyo maana tuliamua kwamba ningeanza, na nina furaha sana," **Lionel Messi, ambaye juzi alirejea uwanjani akitokea chumba cha majeruhi na kufunga mabao mawili na pasi ya mwisho moja, hivyo kuiwezesha Inter Miami kushinda 3-1 dhidi ya Philadelphia Union. Messi ana mabao 14 katika mechi 13 alizocheza.**



"Si kwa mchakato, lakini ni kikwazo kikubwa, ukipoteza mchezo wa nyumbani huwa ni kikwazo, haswa tukikutana na timu, hatuijui, labda watapigania nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa, lakini kawaida timu hii haiishii kwenye 10 bora," **Kocha wa Liverpool, Arne Slot, baada ya timu yake kukubali kichapo cha bao 1-0 nyumbani juzi dhidi ya Nottingham Forest, ikiwa ni mara ya kwanza kufungwa na timu hiyo hapo Anfield tangu Februari 1969, shukrani kwa mtunguaji Callum Hudson-Odoi.**



"Nadhani atafanya vizuri, kusema ukweli, muundo wa klabu ni mzuri, mzuri na imara. Wana kocha mkuu na rais ambaye amekuwapo miaka mingi sana, sidhani litakuwa suala kubwa kwake, kwa sababu kipaji chake - ameonesha kila kitu ambacho kinaweza kufanya hivyo. Kwa maoni yangu, anaweza kuwa mshindi wa Ballon d'Or miaka ijayo. Yeye, pengine Erling Haaland, Jude Bellingham, Lamine Yamal... Nadhani kizazi hiki kipya, wana mengi, lakini naamini Mbappe atafanya vizuri sana," **Cristiano Ronaldo ambaye hivi karibuni alifikisha mabao 900, akimtabiria makubwa Kylian Mbappe ndani ya Real Madrid.**





DUBE

# SURA MBILI ZA DUBE YANGA NA KELELE ZA KUKOSA MABAO

Na Adam Fungamwango

UNAWEZA kufunga zaidi ya wengine, lakini huwezi kufunga kila mechi na kuweka mpira wavuni kila nafasi inayopatikana.

Mijadala imekuwa mikali kuhusu kiwango cha straika wa Yanga, Prince Dube, baada ya kumalizika kwa mchezo wa mkondo wa kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya raundi ya kwanza, uliochezwa Uwanja wa Abebe Bikila nchini Ethiopia dhidi ya wenyeji, CBE.

Licha ya kufunga bao pekee katika mchezo huo, lakini ndiye aliyekosa mabao mengi ya wazi katika mchezo huo.

Alikosa mabao manne, lakini matatu yakionekana ni rahisi zaidi kukosa kuliko kupata.

Pamoja na ushindi wa bao 1-0 ugenini, lakini mijadala kwenye mitandao ya kijamii, kwenye vijiwe vya michezo, redioni na televisheni, imekuwa ni jinsi Yanga ilivyokosa mabao mengi, hasa straika huyo raia wa Zimbabwe.

Baadhi ya mashabiki wa Yanga jana walionekana kutoridhishwa na mwenendo wake wa kukosa mabao, wakikumbushia hata kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar.

Hata hivyo, pamoja na Dube kwa siku za karibuni kuonekana kukosa mabao mengi, rekodi na takwimu zinambeba, kwani yeye na Stephane Aziz Ki, ndiyo wachezaji waliofunga mabao mengi ya Yanga mpaka msimu huu, tangu kuanza kwa msimu huu, akianzia kwenye michezo ya kirafiki ya kimataifa 'pre season', hadi mechi za kimashindano ikiwamo ya juzi.

Haya ndiyo mabao ya Dube aliyopachika akiwa na Klabu ya Yanga baada ya kujiunga nayo msimu huu akitokea Azam FC.

**TS Galaxy vs Yanga**

Alifunga bao kwa mguu wa kushoto akiwa kwenye wingi ya kushoto dakika ya 55, dhidi ya TS Galaxy ya Afrika Kusini katika mchezo maalum wa kimataifa kugombea Kombe la Mpumalanga Julai 24, mwaka huu, Uwanja wa Mbombela nchini Afrika Kusini. Lilikuwa bao la kwanza kwa straika huyo akiwa na klabu hiyo. Yanga ilishinda bao 1-0.

**Kaizer Chiefs vs Yanga**

Katika mchezo mwingine wa kimataifa Yanga ikiwa Afrika Kusini, Dube alipachika bao moja katika mchezo wa Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chiefs, uliochezwa Julai 28, mwaka huu, Uwanja wa Bloemfonteim.

Alifunga dakika ya 24 baada ya mabeki wa timu mwenyeji kujichanganya wenyewe na kuukwamisha kwa mguu wa kulia, Yanga ikishinda mabao 4-0, mengine yakipachikwa na Stephane Aziz Ki, aliyefunga mawili na Clement Mzize moja.

**Yanga vs Azam FC**

Ilikuwa ni Agosti 11, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, katika mchezo wa fainali ya Ngao ya Jamii, Yanga ikishinda mabao 4-1 dhidi ya Azam FC.

Katika mabao hayo, Dube pia alitupia moja, lililokuwa la kusawazisha baada ya Feisal Salum kutangulia kufunga bao dakika ya 13.

Alitanguliziwa mpira mrefu, kama kawaida yake akawaacha kwa mbio, mabeki wa Azam, akaupachika wavuni kwa mguu wa kulia, dakika ya 19.

Mabao mengine ya Yanga katika mchezo huo yalifungwa na Aziz Ki, Mzize, Yoro Diaby akijifunga mwenyewe.

**Vital'O vs Yanga**

Alifunga kwa mguu wa kushoto likifanana kabisa na lile alilofunga dhidi ya TS Galaxy ya Afrika Kusini.

Ilikuwa ni Agosti 17, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, katika mchezo wa hatua ya awali, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vital'O ya Burundi.

Aliupata mpira kwenye wingi ya kushoto kama kawaida yake, akaingia ndani kidogo akaukwamisha wavuni dakika ya sita ya mchezo. Katika mchezo huo Yanga ilishinda mabao 4-0, mengine yakifungwa na Aziz Ki. Clatous Chama na Mzize.

**Yanga vs Vital'O**

Dube alifunga tena bao katika mchezo wa marudiano Ligi ya Mabingwa Afrika hatua za awali dhidi ya Vital'O ya Burundi, mechi ikichezwa tena Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, na Yanga kushinda mabao 6-0.

Katika mchezo huo uliochezwa, Agosti 24, mwaka huu, mabao mengine yalifungwa na Pacome Zouzoua, Mzize, Chama, Aziz Ki na Mudathir Yahaya.

Dube, alifunga kwa mguu wa kulia akitokea upande wa kushoto ambako ndiko anapendelea zaidi kutegea mipira yake, aliingia nao ndani kidogo, akaupiga kwa mguu wa kulia na kujaa nyavuni.

**JE, WAJUA?**



MABAO mawili aliyofunga Erling Haaland wakati wakishinda 2-1 juzi dhidi ya Brentford Jumamosi iliyopita, yanamfanya kwa ujumla kuifungia timu hiyo mara 99 katika mechi 103 alizocheza kwenye Ligi Kuu England. Ili kuweka hilo katika muktadha, mshambuliaji, Sergio Aguero alichukua michezo 390 kuweza kuweka rekodi yake kwa klabu hiyo ya mabao 260. Kwa kiwango cha sasa cha Haaland kitambadilisha Muargentina huyo ndani ya misimu mitatu.



## Ujenzi tangi la gesi Soko la Samaki Feri waiva

**Na Gwamaka Alipipi**

MBUNGE wa Ilala, Mussa Zungu, amesema wamefikia makubaliano ya kisheria na kampuni ya Oryx Gas Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa tangi la kisasa la gesi katika Soko la Kimataifa la Samaki la Feri jijini Dar es Salaam, ambalo litagharimu Sh.milioni 300.

Akizungumza wakati wa kutambulisha mradi huo Zungu alisema wafanyabiashara hasa wakaanga samaki katika soko hilo wamekuwa wakipata hasara ya kununua mitungi ya gesi.

Alisema lakini kati ya mitungu hiyo ni asilimia 45 tu ndiyo inafanya kazi kutokana na mazingira ya gesi kuganda na kuwa barafu.

Zungu alisema hatua hiyo ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kutunza mazingira, kwamba moshi wa kuni na mkaa unaharibu mazingira.

"Tunawashukuru sana kampuni ya Oryx Gas nchini ambayo imekubaliana kwa pamoja kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kusaidia kundi hili la wafanyabiashara wakaanga samaki wapate nishati safi na salama lakini kwa gharama ya fedha wanazotoa," alisema Zungu.

Alisema hatua walizochukua kisheria zimekamilika kwa asilimia 90 na hayo yote wanayofanya ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwatazama wananchi kwa jicho la huruma, kuhakikisha kila mwananchi anafanya shughuli zake kibiashara kwa gharama ya chini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Ashelly Mbasha, alisema: "Tunachokiomba ni ulinzi wa miundombinu mradi utakapoanza kwani tunaweka miundombinu ya gharama kubwa kwa kuwa gesi inataka usalama mkubwa".

Alisema wataendelea kushirikiana na serikali, alimshukuru Mbunge wa Ilala kwa kuja na ubunifu huo.

Mbasha alisema makubaliano ya awali yameshafikiwa na sasa wako katika hatua za mwisho na hatimaye kuanza utekelezaji wa mradi. Hivyo alishukuru kwa hatua hiyo na kubwa, akiomba ushirikiano wa wafanyabiashara wa soko hilo na wadau ili mradi ukamilike kwa muda uliokusudiwa.

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto, alisema: "Zungu anafanya kazi kubwa ya kumsaidia Rais Samia na hayo yanayofanyika katika soko hilo yanatokana na kupokea maelekezo kutoka kwa Rais Samia ya kuhakikisha wanabadilisha matumizi ya kuni na mkaa na kuingia katika matumizi ya gesi".

# Viongozi Soko la Machinga kikaangoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewasimamisha viongozi wa Soko la Machinga jijini Dodoma, ili kupisha uchunguzi kutokana na tuhuma zinazowakabili ikiwamo kughushi barua za Mkurugenzi wa Jiji.

Alitoa uamuzi huo juzi alipokuwa akitatua kero za wafanyabiashara katika mkutano wa hadhara aliofanyika sokoni hapo.

Katika mkutano huo wafanyabiashara walipata fursa ya kuwasilisha kero zao kwa kiongozi huyo na kumweleza madai ya viongozi wa soko ambao ni Mwenyekiti na Meneja kwamba wanauza vizimba kinyume na taratibu, pia kughushi barua za Mkurungenzi wa Jiji pamoja na vitambulisho vya wajasiriamali.

Kutokana na shutuma hizo, Rosemary alisema: "Zipo tuhuma za kiuongozi lakini nyingine za jinai kama kufoji vitambulisho na barua. Hatuna uhakika mpaka uchunguzi ufanyike. Wakati uchunguzi unafanyika Mwenyekiti na Meneja wasimamishwe kwani wameonekana ni sehemu ya tatizo."

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri, alisema awali aliunda timu ya uchunguzi ikiongozwa na Mkuu wa TAKUKURU Wilaya na moja ya kero ilikuwa ni ulipaji ushuru wa siku.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Dk. Fredrick Sagamwiko, alisema ofisi yake ipo mbioni kukamilisha mfumo mpya wa uendeshaji wa soko ambao unatarajiwa kuanza Oktoba mwaka huu ambao utakwenda kutatua kero zote za wafanyabiashara hao.

Alisema kuanzia Septemba 17, 2024, wataanza uhakiki wa kupata idadi kamili ya wafanyabiashara wenye vizimba katika soko hilo.

# THBUB yaingilia kati matukio wananchi kuchukua sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imewaasa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na kuwaomba viongozi wa ngazi zote kutoa elimu, ili watu watambue umuhimu wa maisha ya binadamu.


Rai hiyo imekuja siku chache baada ya tukio lililotokea mkoani Geita wananchi kuwashambulia watu wawili waliokuwa wamebeba watoto wakidhani wameibiwa, hali iliyosababisha kuzuka kwa vurugu kwenye kituo cha polisi.

Vurugu hizo zilisababisha kuchoma moto gari ambapo watu wawili walifariki dunia kwenye tukio hilo.

Mwenyekiti wa THBUB, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye hafla ya uzinduzi wa basi la THBUB litakalowasaidia watumishi wake katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema vitendo vya kujichukulia sheria mkononi siyo ustaarabu kwa kuwa Tanzania ni nchi ya kistaarabu, hivyo ustaarabu huo unataka wananchi wawe wanafanya kila jambo kwa kuzingatia utawala wa sheria.

Akizindua gari hilo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi, aliwaasa wananchi kuunga mkono jitihada zinazofanywa na THBUB kwa kutoa taarifa zilizo sahihi, ili kusaidia katika uchunguzi unaofanywa na tume hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Suleiman Mwenda, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kisana, kata ya Kisiriri juzi, kwenye mkutano wa hadhara ambao ulikuwa maalum kwa ajili ya kusikiliza kero na kuzipatia ufumbuzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wafamasia Jumuiya ya Madola watoa elimu ya UVIDA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na ongezeko la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (UVIDA), wafamasia kutoka Jumuiya ya Madola kwa kushirikiana na Shirika la THET wameanza kutoa mafunzo ya kukabiliana na tatizo hilo kwa wafamasia katika hospitali mbalimbali nchini.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mratibu wa Mradi wa CwPAMS 2.0, Benard Makala, alisema wanaendesha mafunzo ya kuzuia na kudhibiti maambukizi (IPC) kama sehemu ya kupambana na vimelea sugu vya magonjwa.

Makala ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma alisema mafunzo hayo yalianza mwaka jana katika hospitali mbalimbali za mikoa ya Dodoma, Katavi, Kilimanjaro na Mbeya ambako wamepata matokeo mazuri.

Akizungumza na watumishi na wafamasia wa Hospitali ya St Gemma jijini Dodoma, Makala alisema kwa sasa kuna mzigo mkubwa wa maambukizi ya magonjwa yanayopatikana kwenye vituo vya afya na maeneo yanayotoa huduma za afya nchini.

"Tanzania ilikumbwa na maambukizi ya usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa yatokanayo vituo na ambapo inakadiriwa kuwa takribani vimelea milioni 1.29 vilitokea kwa mwaka 2020," alisema Makala.

Alisema mafunzo yanayotolewa yanajumuisha mazoea ya jumla ya IPC, matumizi sahihi ya vitakasa mikono ili kuhakikisha mradi huo unadumu na unakua endelevu na kuwapatia malighafi na vifaa vya kutengenezea vitakasa mikono hospitalini hapo.

Kwa mujibu wa Makala, mafunzo hayo ni sehemu ya mradi mkubwa wa CwPAMS 2.0 ambao unatekelezwa kwa ushirikiano na Northumbria Healthcare ya Uingereza na Kilimanjaro Christian Medical Centre.

Alisema hospitali tisa zilizonufaika na mpango huo ni Dodoma Christian Medical Center, Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, Igawilo, Viwawa, Hospitali ya Barali na JKCI ya jijini Dar es Salaam.

Mfamasia Mkuu katika Hospitali ya St. Gemma, Ambrose George, alikiri kuwa mafunzo hayo licha ya kuwa ni ya muda mfupi, lakini yamekuwa msaada mkubwa kwani wahusika wanajifunza kwa vitendo moja kwa moja.

Ambrose alisema mbali na mafunzo ambayo wanapewa na taasisi hiyo lakini walikabidhiwa malighafi za kutengeneza vitakasa mikono na kukabidhwa vifaa katika maeneo 10 ya muhimu katika hospitali hiyo.

Alisema wataendelea kufundisha wataalamu wengine ambao hawakupata nafasi ya kujifunza hapo, ili kupunguza tatizo la maambukizi ya vimelea kwa wafanyakazi wao na wagonjwa wanaopata huduma.



# TANAPA yabuni mkakati mpya utatuzi migogoro na wafugaji

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeanzisha mkakati mpya wa kutatua migogoro kati ya wafugaji na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kukaa vikao vya pamoja kati ya maofisa wa hifadhi hiyo, wafugaji na viongozi wa serikali.

Vikao hivyo vilianza kufanyika mwishoni mwa wiki katika Ofisi za TANAPA Kanda ya Kusini zilizopo wilayani Mbarali ambapo washiriki wa kikao hicho walikuwa ni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbarali, wawakilishi wa wafugaji, maofisa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Washiriki wengine walikuwa ni maofisa wa TANAPA Kanda ya Kusini na maofisa wafugaji wa kata 11 zinazopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, alisema Bonde la Usangu ambalo liko ndani ya hifadhi hiyo limekuwa likivamiwa na mifugo, hali ambayo inahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.

Alisema bonde hilo ni chanzo cha maji cha Mto Ruaha ambao ni muhimu kwa ajili ya viumbe hai vilivyomo ndani ya hifadhi pamoja na uzalishaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera, Kidatu na la Mwalimu Nyerere.

Alisema ikolojia ya bonde hilo ni muhimu kwa utalii kutokana na kuwa kivutio kwa makazi ya viumbe mbalimbali wakiwamo wanyama, mimea na ndege adimu.

Vilevile alisema kitendo cha wafugaji kuingiza mifugo hifadhini kinasababisha mabadiliko ya tabia za wanyamapori wanaokula nyama kama simba na chui kuanza kuwinda mifugo badala ya wanyamapori.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Maulid Surumbu, alipongeza uongozi wa TANAPA kwa kubuni mbinu hiyo ya vikao, akisema itasaidia kutatua migogoro na kero bila kuwapo wa vurugu.

Pia, aliwaomba wahifadhi kutumia vikao hivyo kuwaelimisha wafugaji kuhusu umuhimu wa kuitunza hifadhi kwa kutoingiza mifugo hifadhini, huku akiwataka wafugaji kuzingatia elimu hiyo kwa faida yao na hifadhi.

Kadhalika, aliwataka wafugaji wilayani humo kusoma Sera ya Mifugo, sheria, kanuni, miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili wafuge kwa tija na kuepuka migogoro.

Katibu wa Chama cha Wafugaji (CCWT) Wilaya ya Mbarali, Barick Julius, aliomba iundwe kamati maalumu ya kushughulikia mifugo inayokamatwa ndani ya hifadhi kabla ya hatua zingine kali kuchukuliwa ikiwamo kupelekwa mahakamani na kuitaifisha.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, akisikiliza muhtasari wa kuanzishwa Kiwanda cha SukariBagamoyo Sugar kilichoko Makurunge, wilayani Bagamoyo, Pwani alipotembelea kiwandani huko juzi. Anayeelezea ni Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni za Bakhresa Group, Hussein Sufiani. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shule tano za msingi kujengewa madarasa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI imesema inakusudia kujenga madarasa mapya katika shule za msingi Ilunda, Welela, Sovi, Lunguya na Nyamalo zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, ili kutatua kero ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI (Elimu), Zainab Katimba, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika Kituo cha Afya Mtwango wilayani Njombe.

Alisema hatua hiyo ni kutokana na jitihada zinazofanywa na Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwini Swalle ya kuhakikisha miundombinu bora inapatikana katika sekta mbalimbali ikiwamo elimu.

Alisema Novemba 27, mwaka huu kutafanyika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hivyo wananchi wanajukumu la kuchagua viongozi bora watakaokwenda kuwaletea maendeleo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Justine Nyamoga, alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo inawagusa moja kwa moja wananchi.

Diwani wa Viti Maalumu, Kata ya Mtwango, Roida Wandelage, aliiomba serikali kupitia kamati hiyo kuwapelekea mtaalamu wa mionzi pamoja na gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mtwango.

"Mashine ya mionzi ipo lakini hatuna wataalamu, tunaomba mtusaidie mtaalamu awepo kwenye kituo chetu cha afya lakini pia tunamwomba Rais atusaidia gari ya kubebea wagonjwa kwa sababu lililoko ni dogo," alisema Roida.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Chrisphopher Sanga, alisema serikali tayari imeleta vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mtwango.

# Kituo cha afya chapokea msaada vifaa vya mil.20/-

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Musa Kilakala, amepokea msaada wa vifaa kutoka kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One kwa ajili ya Kituo cha Afya Kingolwira.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, Musa aliwapongeza wafanyakazi hao kwa moyo wao wa ukarimu.

Msaada uliotolewa ni magodoro 40, mashine ya kufulia, mashuka 200 na kompyuta mpakato mbili, vyote vikiwa na thamani ya shilingi milioni 20.

"Nawapongeza sana wafanyakazi wa Alliance One kwa kujitoa kwenu namna hii, ikiwa ni sehemu ya msaada wenu kwa jamii, hususani wakati huu mnaposherehekea miaka 20 tangu kuanzishwa kwa saccos yenu hii," alisema.

Hivyo, aliwaasa wafanyakazi hao kujitolea kwao huko kusiwe mara ya mwisho na kwamba wasisubiri tena mpaka miaka 20 mingine ipite ndipo watoe msaada kama huo.

Kadhalika, aliwashukuru na kuwaomba wajenge tabia ya kusaidia jamii inayowazunguka angalau kila mwaka, hasa pale ambapo wametengeneza faida kwenye chama chao cha kukopeshana.

"Serikali mpaka hivi sasa imejenga vituo vya afya na hospitali za wilaya nyingi nchini, ikiwamo ya Wilaya ya Morogoro, ambayo inaenda kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa huu," alisema.

Msemaji wa kampuni hiyo, John Magoti alisema kampuni ya Alliance One iliruhusu wafanyakazi wake kuanzisha saccos hiyo miaka 20 iliyopita.

Alisema kampuni hiyo inaamini kwamba kila jambo linalofanywa na saccos hiyo ni kwa ajili ya kubadilisha maisha ya watu ili iweze kuishi vizuri.

Katibu Meneja wa Dimon Morogoro Workers Saccos, George Msangya, alisema wafanyakazi hao wametoa msaada huo kupitia chama chao hicho na kuongeza kwamba kampuni hiyo hapo awali ilikuwa ikiitwa Dimon, kabla haijabadilisha jina na kuitwa Alliance One Tobacco Limited.

Msangya alisema mbali na msaada wa vifaa hivyo, wafanyakazi hao pia wameshiriki zoezi la uchangiaji damu lililofanyika hospitalini hapo lenye lengo la kuokoa uhai wa wagonjwa wanaolazwa katika kituo hicho cha afya.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Hemedi Kiduba, alisema msaada huo umekuja kwa wakati.

Alisema: "Tunafarijika kwamba kuanzia sasa hatutakuwa tunasafiri umbali mrefu kufuata huduma za kufua mablanketi, mashuka na vitambaa vya hospitali kwa kuwa kwenye msaada huu wametuletea mashine ya kufulia."

Alisema msaada wa kompyuta utasaidia kuongeza uwezo wa kituo hicho kutunza kumbukumbu za kitabibu kwa ufasaha.



## PBZ yajitosa kuongeza idadi ya watalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Arafat Ali Haji, amesema benki hiyo itaendelea kuunga mkono juhudi za serikali na taasisi binafsi katika kuiwezesha Zanzibar kuwa na utalii kila mwezi, badala ya kutegemea msimu maalum wa utalii pekee.

Alisema hayo juzi visiwani hapa baada ya hafla ya makubaliano ya utiaji saini baina ya benki hiyo na uongozi wa Zanzibar International Marathon.

Alisema katika kuunga mkono juhudi hizo benki hiyo imeamua kudhamini mashindano ya mbio za Zanzibar International Marathon, zinazotarajiwa kufanyika Novemba 3, mwaka huu visiwani hapa ili kuzipa thamani na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuongoza mbio hizo.

Arafat, alisema moja ya ajenda kuu ya uchumi wa Zanzibar ni utalii, kwamba utalii ni moja ya ajenda ya uchumi wa bluu visiwani humo.

Alisema afya iliyobora inachangiwa na ufanyaji mazoezi, hivyo shindano hilo ni sehemu ya kuweka mwili imara lakini pia huwakutanisha watu kutoka sehemu tofauti ndani na nje ya nchi.

Alisema Serikali ya Zanzibar imefanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya michezo, ili kuboresha miundombinu hiyo na kuhamasisha wananchi na kukuza vipaji kwa sababu michezo ni sehemu ya uchumi na ni sekta inayokuwa kwa kasi ndani ya mipaka ya Tanzania.

Alisema mbio hizo ni fursa kubwa kwa Zanzibar ambazo zinathamani na zinawakutanisha watu wengi na zinachangia kukuza pato la taifa litokanalo na utalii.

Mwenyekiti wa mashindano hayo, Hassan Mussa, alisema malengo ya mbio hizo ni kuunga mkono mawazo na jitihada za Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema malengo ya mbio hizo ni kuwa sehemu ya kivutio kipya cha utalii kwa Zanzibar na kuongeza kiwango kikubwa cha watalii wanaofika visiwani humo.

PBZ itagharamia baadhi ya huduma katika mbio hizo, ikiwamo kuwezesha upatikanaji wa miundombinu itakayorahisisha shughuli hiyo kufanyika kwa usalama.

# Mfumuko wa bei wapungua kwa asilimia 0.14 Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MFUMUKO wa bei visiwani Zanzibar kwa mwaka ulioisha Agosti, 2024 umepungua hadi kufikia asilimia 5.12 kutoka asilimia 5.26 iliyorekodiwa kipindi cha Julai 2024.

Hayo yalisemwa na Mtakwimu Kitengo cha Takwimu za Bei Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Hassan Jamal Hassan, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema hali hiyo ilichangiwa zaidi na kupungua kwa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na vileo kwa asilimia 8.69 kipindi cha Agosti 2024, ikilinganishwa na asilimia 8.96 kipindi cha Julai 2024.

Alizitaja bidhaa zilizopelekea kupungua kwa mfumuko wa bei mwaka ni pamoja na mchele wa Mbeya (8.7%), mchele wa Basmat (2.9%), unga wa ngano (5.6%), unga wa sembe (8.3%), mafuta ya kupikia (3.3%) ndizi za mkono mmoja (15.2%) na ndizi za mtwike (25.4%) na sukari nyekundu (0.5).

Alisema kwa ujumla faharisi za bei ziliongezeka na kufikia asilimia 112.64 Agosti 2024, ikilinganishwa na asilimia 107.15 ambayo iliripotiwa Agosti 2023.

Alisema mfumko wa bei za chakula wa mwaka ulioshia Agosti 2024, umepungua na kufikia asilimia 8.88 ikilinganishwa na asilimia 9.16 iliyorekodiwa Julai 2024.

Aidha, alisema mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za chakula pia ulipungua na kufikia asilimia 2.32 ikilinganishwa na asilimia 2.37 kipindi cha Julai.

Kwa upande wa mfumko wa bei kwa kipindi cha Agosti 2024, uliongezeka na kufikia asilimia 0.30 ikilinganishwa na asilimia 0.22 iliyorekodiwa kipindi cha Julai 2024.

Aidha, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa Agosti 2024, umeongezeka na kufikia asilimia 0.89 ikilinganishwa na asilimia 0.15 iliyorekodiwa Julai 2024.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kuongezeka kwa mfumuko wa bei ni pamoja na samaki (8.1%) mafuta ya kupikia (OKI) (2.8%) na mafuta ya dizeli (6.0%).




Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Musa Kilakala (wa pili kushoto), akipokea kompyuta mpakato kutoka kwa Dickson Sika ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Dimon Saccos cha kuweka na kukopa cha kampuni ya Tumbaku ya Alliance One ikiwa ni sehemu ya msaada wao wenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa Kituo cha Afya cha Kingolwira. Wanaoshuhudia ni Mrajisi Msaidizi wa Ushirika mkoani huko, Cecilia Sosthenes (kushoto) na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Blasius Lupenza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Z'bar yaandaa utalii wa halal kukuza pato la taifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imendaa maonesho ya utalii wa halal yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 13, mwaka huu visiwani hapa, utalii ambao unazingatia mila na desturi za Wazanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema, utalii halal unakua kwa kasi kubwa duniani.

Alisema Zanzibar ikiwa ni sehemu ya visiwa vinayotegemea kipato kupita sekta ya utalii, serikali imeona ipo haja ya kukuza na kutambua rasmi utalii huo kutokana na fursa nyingi zinazopatikana.

Soraga alisema soko la utalii huo duniani linatabiriwa kuwa na mapato ya kimataifa yanayotarajiwa kuongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 245.78 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 324.96 ifikapo mwaka 2030.

Hivyo alisema ukuaji huo mkubwa unaonesha umuhimu wa Zanzibar kujitayarisha ili kunufaika na soko hilo.

"Utalii wa halal ni moja ya maeneo ya vipaumbele vya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kupanua wigo wa sekta ya utalii pamoja na kuitangaza Zanzibar na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza azma ya kutangaza vipaumbele hivyo ili kuiweka Zanzibar katika ramani ya dunia," alisema.

Aidha, alisema maonesho hayo yamelenga kuwakutanisha wanunuzi, wauzaji, watoa huduma kwenye sekta hiyo pamoja na wadau muhimu wa utalii wa halal ambapo yatasaidia kuitangaza Zanzibar na kusaidia kuionesha na kutangaza kuwa Zanzibar ni sehemu bora na kivutio muhimu cha utalii huo.

Alisema malengo mingine ni kuwavutia wageni, ukuaji wa uchumi, kupanua masoko ya utalii, kuimarisha biashara za ndani, kukuza utalii wa maadili endelevu na kuongeza sifa ya Zanzibar kimataifa.

"Vilevile tunatarajia kuwa na wanajopo 16 ambao ni wataalamu waliobobea katika fani hiyo ya utalii wakiwamo kutoka Tanzania na nchi tofauti duniani kama vile Afrika Kusini, Uturuki, Uingereza, Indonesia, Croatia na Malta ambao watawasili Oktoba 11 mwaka huu na kufanya ziara katika maeneo mbalimbali ya kihistoria na vivutio vya utalii," alisema.

Hata hivyo alisema Oktoba 12 kutakuwa na tukio kubwa la kihistoria la mwangaza juu ya mwangaza litakalofanyika katika Uwanja wa Amani Unguja ambalo litahudhuriwa pia na kiongozi wa dini Mufti Ismail Ibni Musa Menk na wenzake.

Naibu wa Mufti Mkuu Zanzibar, Mahmoud Musa Wadi, alisema utalii halal unashabihiana na mila na desturi na maadili ya Zanzibar na dini imejiridhisha na utalii huo, hivyo ofisi ya Mufti itaungana pamoja na Kamisheni ya Utalii katika maonesho hayo.

Katibu Mkuu wa Kamisheni ya Utalii, Hafsa Mbamba, alisema wamejipanga kuweka mazingira mazuri ya kufanikisha maonesho hayo na kuwahudumia wageni watakaohudhuria ili nchi kupata mafanikio.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 178 LA 2024**
**BUILD DSM (T) LTD ......MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMMANUEL LUCIAN DAFAY.....MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**EMMANUEL LUCIAN DAFAY**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

BUILD DSM (T) LTD amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinodnoni (mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 16/10/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 09 Mwezi 09 , 2024

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 19984 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU FLORA PETER MAKA**
**NA RACHEL KUYA......MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 03 Mwezi kumi, 2024. Saa 10:00 asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji S.D. MWAIPOPO.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 12 Mwezi 12 Mwezi wa tisa, 2024

NAIBU MSAJILI
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR-ES-SALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**
**KUM:IMM/PW/756/30**



**OMBI LA URAIA WA TANZANIA LA NDUGU CLIMENT MAXINE MUHIRE**

Mtajwa hapo juu ameomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa mambo ya Ndani ya nchi.

Kwa sasa ni raia wa nchi ya BURUNDI Muombaji ni muajiriwa wa kampuni ya ......yenye anuani S.L.P....30000... akiwa yupo nchini tangu mwaka 1995

Kwa yeyote mwenye taarifa ya sababu za kwanini muombaji asipewe uraia wa Tanzania anaombwa atume taarifa kwa njia ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 1181 DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 167 YA MWAKA 2024**
**BAINA YA**
**JENIPHER EMMANUEL RWEYEMAMU ...... MDAI**
**DHIDI YA**
**EDGA LIVING MWAMBAPA .......... MDAIWA**

**KWA:**
**EDGA LIVING MWAMBAPA**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 03.10.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa ajili ya kutaja.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 ya mwezi Septemba, 2024.

MWENYEKITI
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JEREMA LUKASI KIPARA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No.S0888-0099 Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari LANG'ATA BORA Mwaka 2021. Kwa yeyote atakayeiona atoe, Taarifa kituo chochote cha polisi **PHQ/ KIL/MWA/21774/2024**

---

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KINONDONI**
**AT MWANANYAMALA**
**APPLICATION/MISC.**
**APPLICATION NO. 302 OF 2024**
**MMCL FINANCE LIMITED & ANOTHER.............APPLICANT**
**VERSUS**
**MICHAEL JOHN MOMBO & ANOTHER............RESPONDENT**

**SUMMONS/NOTICE**

TO: 1. MICHAEL JOHN MOMBO
2. BONIFACE JUMA LUCHEJA

Take notice that the above matter is coming for mention on 25th September, 2024 before the Hon. J.W. SILLAS chairman of the tribunal. You are hereby commanded to appear at 3:00 noon when the case will be mentioned/heard.

Given under my hand and seal of this tribunal this 26th day of AUGUST, 2024

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 20387 of 2024**
**In the matter of the estate of the late TASMAN LADISLAUS MSANZU KINIGWA of CHAMWINO AREA, IN THE CHAMWINO DISTRICT AND REGION OF DODOMA.**
**AND**
**In the matter of application for letter of administration by HELENA FIDELI MAIGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 11th Day of October 2024.

Dated at Dodoma this 13th Day of September 2024

......... RESIDENT MAGISTRATE .........

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**GODFREY MWITA MANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1293-0031 kilichotolewa na baraza la mitinani la taifa kupitia **IKORONGO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0552-0537 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAGOTO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/93823/2024**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Piga Simu 0677020701

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Sudan Kusini yaahirisha uchaguzi hadi 2026

**JUBA,** Sudan Kusini

SERIKALI ya Sudan Kusini imeamua kuahirisha uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Desemba mwaka huu, na kwamba utafanyika tena baada ya miaka miwili ifikapo 2026 mwezi kama huo.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana kwenye mitandao ya kijamii, na kwamba uamuzi huo umetolewa baada ya kufanyika mkutano wa ofisi ya rais inayojumuisha Rais Salva Kiir Mayardit na makamu wake watano.

Ilielezwa kuwa uchaguzi huo ambao utakuwa wa kwanza katika nchi hiyo changa zaidi duniani, pia uliahirishwa kwa miaka miwili mwaka 2022 ulipopangwa kufanyika.

Tangazo hilo lilitolewa kupitia mtandao wa Facebook na ofisi ya Rais wa Sudan Kusini, lilisema ahirisho hilo linatokana na haja ya muda zaidi kutekeleza kazi muhimu za makubaliano ya amani. Mkataba huu, uliotiwa saini mwaka wa 2018 ili kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoanza mwaka 2013, unatoa fursa hasa kuunganishwa kwa vikosi vya kijeshi, au hata kuandikwa kwa Katiba ya kudumu ya nchi.

Waziri wa Masuala ya Baraza la Mawaziri, Martin Elia Lomuro, alihalalisha ahirisho hilo kwa kutaja mapendekezo kutoka kwa taasisi zote za uchaguzi na sekta ya usalama pamoja na kazi muhimu zaidi zinazohitajika ili kufanyika vizuri kwa uchaguzi.

Tume inayosimamia utekelezaji wa makubaliano ya amani inabainisha katika ripoti yake ya hivi punde kwamba masharti hayajatimizwa kwa uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika kufanyika.

Ilielezwa kuwa katiba ya kudumu ya Sudan Kusini bado haijaandaliwa na vikosi vya jeshi vilivyoungana kwa kiasi kikubwa havifanyi kazi. Na kuna ukosefu wa fedha zinazohitajika kufanya uchaguzi.

Pia inatajwa kuwa kinachoongezwa na hilo ni hali ya kutoamini utawala wa Salva Kiir. Na kwamba watumiaji wengi wa mtandao wanahoji uhalali wa serikali ya sasa, ambayo haijawahi kuchaguliwa na kushutumiwa kwa kutaka kusalia madarakani.

"Ninaweka dau kuwa baada ya miaka miwili, uchaguzi utaahirishwa tena," aliandika mtumiaji wa mtandao baada ya kuona chapisho la ahirisho hilo.

Hata hivyo, wadau walieleza kuwa nia mbaya au shida zisizoweza kuvumilika, pamoja na upanuzi huo mpya wa kipindi cha mpito unaonyesha, kwa mara nyingine tena, jinsi mchakato wa amani wa Sudan Kusini ulivyo mgumu. **RFI**

# Watatu wauawa na milipuko Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

TAKRIBANI watu watatu wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa katika milipuko miwili ya mabomu iliyotokea katika mji mkuu wa Somalia, Mogadishu, ambayo pia ilisababisha uharibifu wa miundombinu.

Ilielezwa kuwa mabomu hayo, ambayo yalilipuka Jumamosi jioni, yalitegwa kando ya barabara kuu kati ya wilaya za kusini mashariki mwa Mogadishu za Dharkinley na Kahda, njia ambayo hutumiwa mara kwa mara na wenyeji.

Ofisa wa usalama mjini Mogadishu alisema, kwa sharti la kutotajwa jina kutokana na vikwazo vya vyombo vya habari, kwamba idadi ya vifo inaweza kuongezeka kutokana na idadi ya watu wanaotumia barabara hiyo.

Alisema vikosi vya usalama vilikimbia hadi eneo la tukio, na kuzingira barabara kwa ajili ya trafiki na kufanya uchunguzi.

Pia ilielezwa kuwa hakuna kundi ambalo limedai kuhusika na milipuko hiyo miwili, lakini kundi la kigaidi lenye mafungamano na Al Qaeda la Al Shabab lilidai kuhusika na mashambulizi kama hayo katika mji mkuu katika siku za hivi karibuni.

Somalia imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa usalama kwa miaka mingi, huku vitisho vikuu vikitoka kwa Al Shabab na makundi ya kigaidi ya Daesh.

Tangu 2007, Al Shabab imekuwa ikipambana na serikali ya Somalia na Kikosi cha Mpito cha Umoja wa Afrika nchini Somalia (ATMIS) na ujumbe wa pande nyingi ulioidhinishwa na Umoja wa Afrika na kuamriwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN).

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kundi hilo la kigaidi limeongeza mashambulizi tangu Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamoud kutangaza vita vya kila namna dhidi ya kundi hilo.

**TRT**




Polisi wakifuatilia chanzo cha milipuko miwili iliyotokea katika mji mkuu wa Somalia Mogadishu, ambako hadi jana hakukuwa na kundi lolote la kigaidi lililodai kuhusika na milipuko hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Raia wa Marekani, Uhispania na Czech wakamatwa Venezuela

**CARACAS,** Venezuela

MAMLAKA nchini Venezuela imewakamata Wamarekani watatu, Wahispania wawili na raia mmoja wa Czech, wanaotuhumiwa kuhusishwa na njama inayodaiwa kulenga kuhatarisha usalama wa nchi hiyo.

Caracas ilibainisha hayo jana, ikieleza kwamba pia kumekamatwa bunduki 400 zinazodaiwa kutoka Marekani ambayo uhusiano wake na Venezuela ni mbaya, ambako saa chache baada ya tuhuma hizo ilikanusha kuhusika na njama hizo zinazolenga kumpindua Rais Nicolas Maduro.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Venezuela Diosdado Cabello, alisema Rais Maduro, ambaye alichaguliwa tena Julai 28, mwaka huu na kupingwa na upinzani na sehemu ya jumuiya ya kimataifa, ndiye aliyelengwa na mpango huo pamoja na maofisa wengine wakuu.

Cabello alihusisha mpango huo unaoshukiwa na idara za ujasusi za Uhispania na Marekani, pamoja na kiongozi wa upinzani Maria Corina Machado.

„Waliwasiliana na mamluki wa Ufaransa, (...) mamluki kutoka Ulaya Mashariki na wanafanya operesheni ya kujaribu kushambulia nchi yetu, na wafungwa waliokamatwa na kuwekwa gerezani wamekiri,“ alisema.

"Bunduki zaidi ya 400 zilizokamatwa zilikusudiwa kwa vitendo vya kigaidi hapa Venezuela, ugaidi unaohimizwa na sekta za kisiasa, tunajua hata serikali ya Marekani inahusishwa na operesheni hii," alisema.

Diplomasia ya Marekani ilijibu kupitia msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, baada ya kufahamishwa kuhusu kuzuiliwa na Caracas kwa askari wa Marekani na kurejelea taarifa ambazo hazijathibitishwa juu ya kuzuiliwa kwa raia wengine wawili wa Marekani.

"Kudai kwamba kuna ushiriki wa Marekani katika njama ya kumpindua Maduro ni uongo kabisa. Marekani inaendelea kuunga mkono suluhisho la kidemokrasia kwa mzozo wa kisiasa nchini Venezuela," msemaji huyo aliandika katika barua pepe.

Kukamatwa kwa watu hao kunakuja huku kukiwa na mvutano mkubwa kati ya Venezuela na Marekani, pamoja na Uhispania, kuhusu uchaguzi wa Rais Maduro ambao ulikuwa na utata.

**RFI**

## HABARI MICHEZO

# KOCHA AZAM FC AJITETEA PAMBA KUMKARIBISHA KWA SARE LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Azam FC, Rachid Taoussi, raia wa Morocco, amesema umaliziaji mbaya na kuchelewa kwa baadhi ya wachezaji waliokwenda kuzichezea timu zao za taifa katika michezo ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), ndiko kulikosababisha kutoka suluhu juzi dhidi ya Pamba Jiji FC.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, kocha huyo alisema bado ana muda mfupi kwenye kikosi hicho na kwamba bado anakiandaa ili kicheze kwa jinsi anavyotaka yeye.

“Tulikuwa tunataka kushinda, lakini si rahisi, kwa siku tano bado tunafundisha jinsi ya kushambulia na kumalizika nafasi, nimefurahi kipindi cha kwanza tumefanya vizuri sana, tumeshambulia kama nilivyokuwa nataka, tatizo letu lilikuwa kwenye kumalizia.

Kingine ni kwamba wachezaji wetu walichelewa kujiunga kutoka kwenye vikosi vya timu ya taifa, kwa muda wa siku kadhaa hawakuwa kwenye mikono yangu, hii nayo imeathiri sana mipango yangu kwenye mchezo wa leo,“ alisema Taoussi.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara kwa kocha huyo ambaye ameichukua timu kutoka kwenye mikono ya Msenegal Youssouph Dabo, aliyeoneshwa mlango wa kutokea baada ya kikosi hicho kusukumizwa nje ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali dhidi ya APR, pamoja na kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania.

Naye Kocha wa Pamba Jiji, Goran Copunovic, ameeleza kufurahishwa na jinsi vijana wake walivyopambana, hasa kipindi cha pili.

“Tumecheza vema, hasa kipindi cha pili, tumewashambulia sana wapinzani wetu, timu yetu ndiyo kwanza imepanda daraja, tulikuwa tunacheza na timu kubwa, yenye uzoefu kwenye Ligi Kuu, iliyotoka pia kucheza mechi za kimataifa, tulistahili ushindi au sare tuliyoipata,“ alisema kocha huyo raia wa Serbia.

Matokeo ya mechi ya juzi, yameifanya Pamba Jiji kushika nafasi ya nane kwenye msimamo ikiwa na pointi tatu na michezo mitatu, Azam ikiwa ya 10, ambapo ina pointi mbili na mabao mawili mpaka sasa.

**HAT-TRICK...**



Mshambuliaji wa Bayern Munich, Harry Kane, akiifungia timu yake moja kati ya mabao matatu aliyofunga juzi wakati wakiibuka na ushindi wa 6-1 ugenini dhidi ya Holstein Kiel, kwenye mechi ya Bundesliga. **PICHA: MTANDAO**

# Kocha Mlandege ataka muda zaidi kuisuka

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Timu ya Mlandege FC, Hassan Ramadhan, amesema bado anahitaji kuki-boresha zaidi kikosi chake ili kuhakikisha anapata matokeo mazuri hasa ya pointi tatu.

Mlandege FC hadi sasa ina alama mbili baada ya kutoka sare michezo yake miwili ya Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema bado hajaridhika na uchezaji wa timu yake hasa katika safu ya ulinzi na ushambuliaji.

Alisema timu yake inashambulia vizuri, lakini inashindwa kupata mabao licha ya kutengeneza nafasi nyingi za wazi.

Ramadhan alisema bado anaendelea kutafakari namna bora ya kukabiliana na kasoro zinazoendelea kujitokeza katika michezo miwili aliyoiona.

Kocha huyo alifafanua kuwa makosa yote aliyoyaona katika mchezo wao wa kwanza ndio hayo hayo aliyoyaona katika mchezo wa pili.

“Tunahitaji kuhakikisha tunayafanyia kazi matatizo haya ambayo yanayojirudia, bado naendelea kutofahamu wapi wanakwama, maana nafasi tunazitengeneza na tunazikosa katika ufungaji,“ alisema.

Aidha, alisema ataendelea kuhakikisha wachezaji wake wapya waliosajiliwa msimu huu wanaungana vema na wale wa zamani.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa Mlandege kuwapa muda wachezaji wao ili wafanye vizuri katika michezo ijayo.

## Prisons yaanika sababu kukosa tatu za Tabora

**Na Shufaa Lyimo**

KITENDO cha kupoteza umakini katika mchezo wa Ligi Kuu juzi dhidi ya Tabora United, ndiyo sababu ya kuambulia pointi moja wakiwa ugenini, kwa mujibu wa benchi la ufundi la Tanzania Prisons.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbwana Makata, alisema endapo wachezaji hao wangekuwa makini walikuwa na uwezo wa kupata pointi zote tatu.

"Wachezaji wangu hawakuwa makini katika mchezo huo ndio maana tumeshindwa kutimiza malengo tuliyojiwekea ya kuondoka na alama zote tatu,“ alisema Makata.

Kocha huyo alisema licha ya matokeo hayo hajakata tamaa na badala yake anakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo wao ujao dhidi ya Dodoma Jiji FC.

„Kwa sasa tunakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo wetu ujao, malengo ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu,“ alisema kocha huyo.

Akizungumzia mchezo huo kwa ujumla, alisema ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa na hiyo inatokana na namna timu zilivyokuwa zimekamiana.

"Mchezo ulikuwa mgumu na wenye upinzani, kila timu ilikuwa inataka kupata pointi tatu ndio maana zilikuwa zinacheza kwa kukamiana zaidi,“ alisema.

Matokeo hayo yanaifanya Tanzania Prisons kufikisha pointi tatu zinazotokana na michezo mitatu waliyocheza hadi sasa ikiwa katika nafasi ya nane ya msimamo wa ligi hiyo.

Kwa upande wa Tabora United ambayo imeshuka dimbani mara nne hadi sasa kwenye ligi hiyo, ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama saba sawa na Mashujaa FC ambayo imecheza michezo mitatu sawa na vinara Singida Black Stars wenye pointi tisa kileleni.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADRID WAMTAKA SALIBA

KLABU ya Real Madrid ilituma skauti katika mchezo wa jana Jumapili wa London Kaskazini huku wakifikiria kumnunua beki wa Arsenal mwenye umri wa miaka 23, William Saliba na wa kati wa Tottenham na Argentina, Cristian Romero, mwenye wa miaka 26. (***Defensa Central***)

### CHUKWUEMEKA ALENGWA

WINGA wa Chelsea mwenye umri wa chini ya miaka 20, Carney Chukwuemeka, ni miongoni mwa walengwa wa AC Milan katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Calciomercato***)

### DAVIES AKARIBIA MADRID

REAL Madrid wanakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23, kwa uhamisho wa bila malipo, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada akiwa tayari. (***AS***)

### BADE AWANIWA LIVER

LIVERPOOL inamtafuta mlinzi wa Sevilla Mfaransa Loic Bade mwenye umri wa miaka 24, huku wakifikiria kuchukua nafasi ya mlinzi wa kati wa Uholanzi Virgil van Dijk mwenye miaka 33. (***Caught Offside***)

### OSIMHEN NA CHELSEA

CHELSEA inaweza kurejea kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la Januari kutokana na kipengele cha mauzo katika mkataba wake wa mkopo huko Galatasaray. (***Football Insider***)

### BARCA WALIKATAA

BARCELONA ilikataa ofa ya takriban pauni milioni 210 kutoka kwa Paris St-Germain kwa winga wa Hispania, Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 17, Juni mwaka huu, kulingana na Andy Bara - wakala wa kiungo wa kati wa Barca na Hispania, Dani Olmo. (***Mundo Deportivo***)

### MATIP ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inaendelea kufanyia kazi mpango wa kumsajili beki wa zamani wa Cameroon, Joel Matip mwenye umri wa miaka 33, kwa uhamisho wa bure. (***Football Insider***)

### RABIOT HATAREJEA JUVE

MAMA na wakala wa Adrien Rabiot amesema kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, ambaye amekuwa akihusishwa na Newcastle United na Manchester United, hatarejea kwenye klabu yake ya zamani ya Juventus. (***Mirror***)

### EVERTON KUNUNULIWA

MFANYABIASHARA wa Marekani, John Textor ana imani kuwa dili la kuinunua Everton linaweza kukamilika baada ya wiki nne. (***Guardian***)


### MONGAN ATOSWA MADRID

ANDY Mangan wa Stockport County amezuiwa kujiunga na timu ya makocha ya Real Madrid baada ya kunyimwa kibali cha kufanya kazi kwa sababu ya kanuni za Brexit. (***Times***)

### CHUKWUEMEKA KWA MIKOPO

KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili kwa mkopo winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20 kutoka England, Carney Chukwuemeka. (***Teamtalk***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANCELOTTI: MBAPPE SASA NI MPYA ZAIDI

**MADRID,** Hispania

●●● Ni hatari sana, ukichanganya vema na Vinicius na wengine, anaimarika, nimependa sana...

CARLO Ancelotti alisifu uchezaji wa Kylian Mbappe baada ya fowadi huyo kufunga katika ushindi wa mabao 2-0 wa Real Madrid ugenini dhidi ya Real Sociedad Jumamosi, akisema anaonekana „mpya zaidi, mwenye bidii zaidi" na „anaimarika sana."

Vinicius Junior alitangulia kufunga kwenye Uwanja wa Reale Arena dakika ya 58, kwa mkwaju wa penalti baada ya Sergio Gomez kuunawa mpira, kabla ya Mbappe kuongeza penalti nyingine dakika ya 75 Vinicius alipofanyiwa madhambi.

Katika mechi tano alizocheza Mbappe za LaLiga hadi sasa msimu huu, ana mabao matatu.

„Mbappe anaonekana mchanga zaidi, akifanya kazi zaidi kwenye mpira," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

**"Ni hatari sana, ukichanganya vema na Vinicius na washambuliaji wengine. Anaimarika. Nilipenda mchezo wake sana."**

Ancelotti alisema amewaacha Vinicius na Mbappe kuamua nani apige penalti, huku wote wawili wakiwa wamefunga mara mbili kwenye kampeni hii.

"Kwanza ni Vini ndiye aliyefunga, kisha wakaamua Kylian achukue moja," alisema Ancelotti. „Wanachukua jukumu, na hadi sasa imekwenda vizuri."

Mbappe mwenyewe aliiambia Real Madrid TV kwamba anahisi anazoea mazingira yake mapya.

"Kila mchezo ninajisikia vizuri, ninaelewa kile timu, kocha na wachezaji wenzangu wanahitaji," alisema Mbappe.

"Vinicius na mimi tunajaribu kutafutana kwenye mchezo na katika mazoezi ili kupata muunganisho huo, yeye ni mchezaji mzuri.

"Jambo muhimu ni kwamba penalti nne [hadi sasa msimu huu] zilikuwa mabao, si nani anayezifunga. Tulifunga zote nne, na hilo ndilo jambo muhimu zaidi."

## HABARI MICHEZO

# 'RASHFORD SASA AMEFUFUKA'




**MANCHESTER,** England

ERIKI ten Hag alimsifia Marcus Rashford kuwa na msimu mzuri wa kupachika mabao baada ya mshambuliaji huyo kumaliza ukame wake wa miezi sita Jumamosi kwa kuvumilia shutuma kutoka kwa mashabiki wake.

Rashford alicheza mechi 13 bila bao kabla ya kupachika wavuni dakika ya 41 katika ushindi wa mabao 3-0 wa Manchester kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Southampton iliyopanda daraja, ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu walipo-shinda 2-0 dhidi ya Everton Machi 9, mwaka huu.

Ingawa Ten Hag alikuwa akihojiwa kuhusu kumwanzisha Rashford, alisema kabla ya mchezo huo Jumamosi kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alihitaji bao moja pekee au asisti ili kurudi kwenye kiwango chake.

Ten Hag anaweza tu kutumaini kwamba mchana mzuri utafungua milango kwa mshambuliaji wake, ambaye alikuwa na mabao manane pekee katika michuano yote msimu uliopita baada ya kufunga mabao 30 msimu wa 2022-23, msimu wa kwanza wa Ten Hag huko Manchester.

"Ni muhimu sana," alisema kocha huyo baada ya ushindi wa Jumamosi ulioipa United pointi sita baada ya mechi nne za Ligi Kuu England.

"Kwa kila mshambuliaji, wanataka kuwa kwenye orodha ya wafungaji. Mara ya kwanza anapoingia, zaidi wanakuja."

Mazoezi binafsi wakati wa mapumziko ya hivi majuzi ya kimataifa yalimlipa fowadi Rashford.

Aliachwa nje ya kikosi cha England kwa Euro 2024 na kisha hakuitwa kwa ushindi dhidi ya Finland na Jamhuri ya Ireland.

Baada ya kuanza vibaya msimu polepole, alibaki Manchester wakati wa mapumziko kujifua akitumia muda mwingi kufanya mazoezi ya kumalizia.

# Guardiola: Haaland ni habari nyingine kabisa



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Erling Haaland yuko katika kiwango bora zaidi cha maisha yake Manchester City na alisifu tabia ya mshambuliaji huyo baada ya kufunga mabao mawili dhidi ya Brentford licha ya kushughulika na kifo cha rafiki wake wa karibu.

Haaland aliamua kuanza dhidi ya Brentford Jumamosi licha ya kifo cha rafiki wa familia yao, Ivar Eggja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alifunga mabao yote mawili wakati City ikitoka nyuma na kushinda 2-1 na kufikisha mabao tisa katika mechi nne za kuanza msimu.

„Ningesema kiwango bora zaidi lakini mechi nne tu, si michezo mingi," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

„Sikuuliza kama yuko tayari, kama hakuwa tayari angekuja kwangu, ni silaha ya ajabu, bila shaka imekuwa ngumu. Tunajaribu kumtunza kila mtu hapa na ikiwa mtu ana matatizo tunakaa karibu.

„Lazima uwe na nguvu. Labda kwa dakika 90 usahau maisha yako binafsi ikiwa maisha yatakupiga usoni."

Mabao mawili ya Haaland kwenye Etihad yalikuja baada ya Yoane Wissa kuipa Brentford uongozi baada ya sekunde 22 pekee.

Kikosi cha Thomas Frank kingeweza kufunga tena katika dakika 10 za kwanza kabla ya City kuchukua udhibiti kutoka kwa mshambuliaji wao wa kati raia wa Norway, Haaland.

Haaland nusura afunge hat-trick tatu mfululizo za Ligi Kuu, lakini akanyimwa bao la tatu dhidi ya Brentford wakati shuti lake lilipogonga mwamba kipindi cha pili.

„Natoa sifa kwa Brentford," Guardiola alisema. „Sio rahisi kuimudu. Walistahili kushinda 2-0 au 3-0.

„Kila wanapokuwa na mpira wanatengeneza nafasi. Mipira mirefu, pambano, pasi fupi fupi, kuvunja mistari, pasi za haraka, mpito; ni timu isiyo ya kawaida. Tunateseka tangu waje Ligi Kuu. Michezo yote na Thomas, imekuwa hivyo."

## Slot aonja kipigo cha kwanza Liver

**LIVERPOOL,** England

ARNE Slot alionja kipigo chake cha kwanza akiwa kocha wa Liverpool juzi, Jumamosi wakati timu yake ilipofungwa bao 1-0 na Nottingham Forest kwenye Ligi Kuu England, huku kocha mgeni Nuno Espirito Santo akimshinda Mholanzi huyo katika pambano la kuvutia.

Forest walipata mbinu zao, wakiweka eneo la katikati ya uwanja na kuwasogeza nje wachezaji wakubwa wa Liverpool. Na ingawa wenyeji walipata nafasi nzuri katika kipindi cha kwanza, hawakuwa na bahati mbele ya lango.

"Matokeo hayo yanafadhaisha zaidi, na hatuwezi kufurahishwa na jinsi mchezo ulivyoenda. Ulikuwa ni mchezo wa kuanzia na hatukutengeneza nafasi zozote," alisema Slot.

"Tunapaswa tu kujiangalia - tunapaswa kuwa bora zaidi. Mara nyingi sana tulipoteza mpira karibu na eneo hilo, haikuwa nzuri vya kutosha. Lazima tuwe bora zaidi tukiwa na mpira."

Safu dhabiti ya Forest inaweza kuwa imewaacha Liverpool wakiwa na uhaba wa nafasi, lakini walikuwa maadui wao wakubwa nyakati fulani na wachezaji wa akiba Anthony Elanga na Callum Hudson-Odoi walijumuika na kufunga bao kwenye kaunta na kudai pointi tatu kwa wageni.

"Maamuzi yetu na utekelezaji haukuwa mzuri vya kutosha. Kwa ujumla tulijilinda vizuri, lakini wachezaji wawili wenye kasi walikuja na kuifanya iwe ngumu. Tulichukua hatari kubwa na mwishowe lilikuwa bao zuri sana," aliongeza Slot.

Kocha wa Forest Mreno Espirito Santo alifurahishwa na jinsi timu yake ilivyotekeleza mpango wa mchezo.

"Njia pekee ya kufikia chochote hapa ni ikiwa umejipanga na kufanya kila kitu unachoweza," alisema.

"Unapoanza jinsi tulivyoanza na mawinga wetu Nico Dominguez na Elliot Anderson, juhudi zote za kuwafuatilia mabeki wa pembeni wa Liverpool, ni nguvu kubwa."

Baada ya kupamba na kushuka daraja katika misimu iliyopita, Forest wanajikuta katika nafasi ya nne wakiwa na pointi nane katika michezo minne baada ya kushinda. Liverpool wanashika nafasi ya pili wakiwa na tisa.



"Tunafanya kazi kwa bidii, na ni juu ya kujenga na kuamini wazo hili ambalo unaweza kuliendeleza," Espirito Santo alisema.

HABARI MICHEZO

## Yanga na hesabu CBE kufia Z'bar

INATOKA UKURASA 24

afanya vizuri, tunampongeza kocha wetu Gamondi na vijana wetu, wamefanya kazi kubwa, tuna bao moja la ushindi na la ugenini pia," alisema Hersi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Andrew Mtine, yeye alilia na ukosefu wa mabao mengi katika mchezo huo.

"Tuna timu nzuri, lakini tumepoteza nafasi nyingi, tumefanya kila kitu kwa usahihi, wenzetu wamepata nafasi moja tu kwa dakika 90, ila sisi tumepoteza nyingi, lakini ndiyo mpira, pia niseme uwanja nao haukuwa mzuri sana, tunakwenda kujiandaa na mchezo unaofuata ili tutinge hatua ya makundi," alisema.

## Bodi ya Ligi: Kagoma mali..

INATOKA UKURASA 24

migogoro, badala yake hupelekwa kwenye Kamati ya TFF na baada ya kumalizika wao wanachopewa ni majina tu.

"Sisi hatuna mgogoro wowote, migogoro inakuwa huko TFF ambako ndiko kuna kamati, baada ya kumalizika sisi tunapewa majina tu ya kuwaruhusu, wao ndio wanaosimamia usajili na ndio wanaotoa leseni, kwa hiyo sisi hatuna mgogoro wowote kwenye usajili, tumepewa majina na tumeruhusu," alisema.

Kutokana na hivyo alisema Kagoma anaichezea Simba kwa sababu tayari ana leseni inayomruhusu na kama ingekuwa vinginevyo wangemzuia kama wanavyozuiwa wachezaji wengine.

"Ukimwona Kagoma anacheza kwenye michezo ya ligi maana yake amepewa leseni na TFF, ambao ndio utambulisho. Mle kuna jina la mchezaji, na unaambiwa ataitumikia timu gani, ndiyo maana nasema hakuna anayelalamika kuwa Kagoma amecheza mechi za ligi akiwa hana leseni, wangesema hivyo ndiyo tungepaswa kuulizwa kwa nini tunamruhusu mchezaji aingie uwanjani ikiwa hana leseni."

Klabu ya Yanga, Mwanasheria, Simon Patrick, amesema tayari suala hilo wamelipeleka kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji na bado halijafanyiwa kazi ili kutoa uamuzi.

# NGUSHI GARI LIMEWAKA, AKIOTA KURUDI YANGA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Crispin Ngushi, amefunga bao lake la pili kwenye Ligi Kuu Tanzania, likiwa pekee katika mchezo ambao timu yake ya Mashujaa FC ilishinda 1-0 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge Dar es Salaam, akisema lengo lake ni kufika mbali zaidi, hata kama itakuwa ni kurejea kwenye klabu yake ya zamani, Yanga.

Ngushi, ambaye alijiunga na Mashujaa kwa mkataba wa mwaka mmoja, akitokea timu hiyo aliyoifunga Ijumaa iliyopita, Coastal Union ambako alikuwa akicheza kwa mkopo kutoka Yanga, alisema anashukuru kwa kupachika bao katika mchezo huo ambalo limekuwa la pili katika michezo mitatu tu aliyocheza akiahidi makubwa zaidi msimu huu.

"Siri ni kwamba Mashujaa ninachokipata naridhika nacho, hata Yanga ilikuwa hivyo ila nilikuwa sipati sana muda wa kucheza kama huku, nitazidi kufanya mazoezi kwa bidii ili niweze kufunga zaidi, hata ikitokea timu yoyote kubwa inanitaka, au kurudi Yanga nitashukuru Mungu kwa sababu lengo langu ni kucheza mpira ili niweze kufika mbali," alisema straika huyo.

Alipoulizwa kama kwa moto huo aliouwasha ameingia kwenye kinyang'anyiro cha ufungaji bora, alijibu ni mapema mno kwa sasa kuongelea hilo.

"Kuhusu ufungaji bora, hayo ni mambo ya mbele sana, ila kwa sasa wacha nipambane, kila mechi kwangu ni fainali," alisema.

Kabla ya bao hilo, Agosti 17, mwaka huu alifunga bao moja lililoipa ushindi wa 1-0, Mashujaa FC dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, likiwa ni bao la kwanza kufungwa msimu huu wa ligi 2024/25.

Straika huyo alisajiliwa 2022 na Yanga kutoka Mbeya Kwanza, lakini baada ya kukosa namba, klabu hiyo ilimpeleka Coastal Union kwa mkopo wa mwaka mmoja, ambapo aliumaliza mwishoni mwa msimu uliopita na msimu huu amesajiliwa Mashujaa kama mchezaji huru.




Kiungo wa Yanga, Clatous Chama (kulia), akiwania kumiliki mpira dhidi ya mchezaji wa CBE, kwenye mechi ya raundi ya kwanza mkondo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Abebe Bikila, Ethiopia juzi na wenyeji kulala kwa bao 1-0. **PICHA: YANGA**

# Fatuma ampania Hidaya pambano la Homa ya SGR

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Mwanadada Fatuma Njiwa kutoka Mbagala Zakhiem, Dar es Salaam, amejinasibu kumchapa mpinzani wake, Hidaya Zahoro wa Morogoro, katika Pambano La 'Homa ya SGR', linalotarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwaka huu, kwenye ukumbi wa Tanzanite, uliopo mkoani Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati akiendelea kufanya hamasa ya pambano hilo, alisema amesikia tambo za mpinzani wake na kumtahadharisha awe makini siku hiyo kwani hatakuwa na huruma.

"Nimejipanga vizuri kukutana na mpinzani wangu, nimesikia majitambo yake siku ikifika hata amini kwa kile nitakachokifanya," alisema Njiwa.

Alisema kutokana na maandalizi aliyoyafanya, anaamini atapata ushindi mkubwa lakini ataweza kuwafurahisha mashabiki wake, na kuwataka wajitokeze kwa wingi siku ya pambano hilo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa bondia huyo, Amos Godwin, alisema anamwamini bondia wake huyo hivyo, kuahidi kupata ushindi.

"Kutokana na kiwango alichokuwa nacho mpinzani wake hawezi kufika raundi ya nne kwa kipigo atakachokipata mbele ya mashabiki wake," alisema Godwin.

Aidha, alisema anaendelea kumpa mbinu mbadala zitakazomlinda pindi atakapokuwa ulingoni ili azidi kuimarisha kiwango chake.

Michezo
Nipashe
Jumatatu Septemba 16, 2024



Slot aonja kipigo cha kwanza Liver

UKURASA 22

# YANGA NA HESABU ZA CBE KUFIA ZANZIBAR

## ●●● Gamondi atamba lengo la kwanza limetimia, huku akidai Jumamosi wataimalizia...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema pamoja na kukosa mabao mengi ya wazi, lakini mpango mkakati ulikwenda kama ulivyopangwa, akiwaahidi wanachama na mashabiki wao kuwa kazi itamalizwa mjini Zanzibar, Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, watakapocheza mchezo wao wa marudiano dhidi ya CBE ya Ethiopia.

Baada ya mchezo wa juzi kwenye Uwanja wa Abebe Bikila, jijini Addis Ababa, Gamondi alisema ilikuwa ni siku mbaya kwa wachezaji wake kukosa mabao mengi ya wazi, lakini alichofurahi ni kwamba lengo limefikiwa.

'Lengo lilikuwa ni kuidhibiti CBE isipate ushindi nyumbani kwake, tulitaka sisi tushinde au tutoke sare na ndivyo ilivyokuwa, vingine vyote vilivyobaki tutakaa chini na kuvirekebisha,“ alisema kocha huyo.

Yanga ilipata ushindi wa bao 1-0, lililowekwa wavuni na Prince Dube, ambaye analaumiwa kwa kukosa mabao mengi ya wazi katika mchezo huo wa juzi.

Moja ya bao ambalo alikosa lilimfanya kocha huyo akasirike na kurusha mikono juu kwa hasira, lakini sekunde chache kabla ya mchezo kwenda mapumziko, alisawazisha makosa yake kwa kufunga, hata mwenyewe Dube alishindwa kushangilia, akibakia kuomba msamaha kwa mabao aliyokosa, ambapo Gamondi aliamua kumtoa kipindi cha pili, nafasi yake ikachukuliwa na Clement Mzize.

Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alimpongeza kocha Gamondi na wachezaji kwa kupambana mpaka kupata ushindi katika mchezo ambao alidai ulichezwa kwenye hali ya hewa ambayo si rafiki.

“Kikubwa hapa ni kwamba tunashukuru kwa kupata matokeo ya ugenini, haijakwisha tutakwenda Zanzibar kwa ajili ya mchezo wetu wa marudiano, tunaahidi tut-

INAENDELEA UK. 23





Kagoma

# Bodi ya Ligi: Kagoma mali halali Simba

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imesema inamtambua Yusuph Kagoma kuwa ni mchezaji halali wa Simba kwani ana leseni ambayo imetoka kwenye mamlaka ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), ambao ndiyo wanaowaletea majina na leseni zao kuthibitisha kuwa wako halali na wanaruhusiwa kutumika kwa timu husika.

Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, amesema changamoto kwao kama Bodi ya Ligi ingekuwa kama wamemruhusu mchezaji huyo kucheza bila ya kuwa na leseni, lakini kwa sababu anayo na inamtaja kuwa ni mchezaji wa Simba, basi ana uhalali wote wa kuichezea timu hiyo.

Amebainisha Simba haiwezi kupokwa pointi kwa kumchezesha mchezaji huyo katika michezo yake ya ligi kwa sababu anacheza akiwa amekamilisha taratibu zote, na migogoro yote huwa inatatuliwa kwenye Kamati za TFF, kabla ya wao kuletewa maamuzi yakiwa yamekamilika.

Boimbanda alisema hayo kufuatia utata uliozuka hivi karibuni kwa Klabu ya Yanga, kudai ina mkataba wa miaka mitatu na Kagoma ambaye amesajiliwa pia na Simba, wakisema kitendo hicho kinaonesha kuwa amesajili timu mbili.

"Siamini kama kwa dunia ya sasa kuna usajili wa timu mbili, siku hizi usajili una mifumo yake, mchezaji akiingizwa kwenye mfumo ulioitwa TMS na klabu moja, hakuna namna yoyote kwa timu nyingine inaweza kuingiza tena jina la mchezaji huyo huyo. Sisi kama Bodi tunapewa majina ya wachezaji ambao usajili wao umekamilika, tunaambiwa hawa wanastahili kutumika na timu hii na ndiyo waliopewa leseni na TFF,“ alisema Boimanda.

Alisema kwao huwa hakuna

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >